SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

**RIPOTI MAALUM**
**Uhaba wa watumishi sasa janga la kitaifa**



UKURASA 5

**MAISHA** Jumapili
Nipashe — Baba, Mama na Mwana



Mkate wa nyama una ladha tamu



MAISHA NI NYUMBA
Zijue mbinu za kupambana na mchwa baada ya ujenzi



KATUNIKA



UREMBO ondoa chunusi


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
Jumapili Septemba 26, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580715
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# KIMBUNGA

**•Rais** Samia afagia vigogo TANESCO, REA, Mramba arejea kivingine....

*Endelea ukurasa 2*



Tito Mwinuka



Mkurugenzi Mkuu mpya wa TANESCO, Maharage Chande



Mwenyekiti mpya wa Bodi ya TANESCO, Omari Issa



Kamishna wa Umeme na Nishati Jadilifu, Felschemi Mramba





Rais Samia Suluhu Hassan akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, akitokea New York, nchini Marekani. Picha ndogo: Baadhi ya wananchi waliofika uwanjani hapo kumlaki. **PICHA: IKULU**

## RIPOTI MAALUM
# Elimu bure tatizo kwa wazazi

UKURASA 4

## Corona yaathiri uchangiaji damu salama

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA SI KWA YANGA UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# Bil. 30/- zatolewa ujenzi kituo biashara kimataifa

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema serikali imeanza rasmi ujenzi wa mradi wa Mtaa wa Viwanda na Kituo cha Biashara cha Kimataifa cha Kurasini na tayari Sh. bilioni 30 zimetolewa.

Amebainisha kuwa kampuni tano zimejitoleza kuwekeza kwenye eneo hilo, nne zikitoka nje ya nchi na moja kutoka Tanzania.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa kutia saini makubaliano na Suma JKT kwa ajili ya ujenzi wa ukuta katika mradi wa ujenzi wa Mtaa wa Viwanda na Kituo cha Biashara cha Kimataifa Kurasini.

Waziri huyo alisema mradi huo utajumuisha mambo matano ambayo ni ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, ujenzi wa viwanda vya kutengeneza na kuunganisha bidhaa mbalimbali na ujenzi wa kituo cha kimataifa cha mauzo ya mazao ya kilimo ikiwamo chai, kahawa, korosho na mboga.

Alisema pia patajengwa maghala ya kuhifadhi katika hali ya uasili na ubaridi bidhaa zinazosubiri kusafirishwa na ujenzi wa kituo cha pamoja cha kutolea huduma (One Stop Services Centre) na huduma za kijamii kama vile ofisi, kituo cha afya na migahawa.

Waziri Mkumbo alisema mwaka huu wa fedha serikali imetenga Sh. bilioni 20 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na kwamba fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kujenga ukuta, miundombinu wezeshi ya barabara, maji na umeme.

Alisema watagharamia huduma za mtaalamu mshauri atakayeandaa mpango wa kina wa uendeshaji, kufanya tathmini ya athari za mazingira na usanifu wa kina wa miundombinu.

Alisema mradi huo unatekelezwa kwa mbia kati ya serikali kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA ) na wawekezaji kutoka Sekta Binafsi.

Kiongozi huyo alisema EPZA walishatangaza zabuni ya kukaribisha wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika mradi huo ambao ni: DP World (Dubai); Elsewedy (Misri); Agility (Dubai); Galco (Tanzania); na Shanghai Lingang Group Co. Ltd (China).

Waziri huyo alisema hatua inayofuata ni kwa wawekezaji waliokidhi vigezo vya zabuni kualikwa kuwasilisha andiko la mradi kwa ajili kufanyiwa tathimini na uchambuzi wa kina ili kumpata mwekezaji atakayeshirikiana na serikali katika kutekeleza mradi huo ambao utaanza rasmi Juni mwakani.

Prof. Mkumbo alisema katika mkutano wa ushirikiano kati ya Afrika na China (Sino-Afriva Cooperation) uliofanyika mwaka 2009 jijini Cairo, Misri, pamoja na mambo mengine, Tanzania ilichaguliwa kuwa moja ya nchi nne za Afrika ambazo zingejenga na kuendesha vituo vikubwa vya biashara katika Bara la Afrika.

Alisema katika kutekeleza lengo hilo, serikali ilitenga eneo la Kurasini kwa ajili ya kujenga kituo hicho na uthamini wa eneo na mali ulifanyika mwaka 2013 na malipo ya fidia kukamilika mwaka 2016.

Prof. Mkumbo alisema hadi sasa, serikali imeshalipa jumla ya Sh. bilioni 101 kwa wananchi waliotakiwa kupisha eneo la mradi huo.

"Kufuatia kukamilika kwa malipo ya fidia serikali ilikabidhi rasmi hati ya eneo hilo kwa EPZA Desemba 10, 2019," alisema Prof. Mkumbo na kuitaka Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kuondoa kitega uchumi chao cha malori katika eneo hilo ili ukuta ujengwe.



Mjane wa aliyekuwa Mwandishi wa Habari wa Kituo cha ITV, Mkoa wa Songwe, Gabriel Kandonga aliyefariki kwa ajali ya gari, akiwa ameshikilia jeneza lenye mwili wa mumewe, baada ya kuwasili nyumbani kwa marehemu eneo la Mpemba, Mji Mdogo wa Tunduma, mkoani humo jana, kwa ajili ya kuagwa na baadaye kuzikwa kijijini kwao Hampangala, kata ya Halungu, wilayani Mbozi. **PICHA: NEBART MSOKWA**


SHREE SANATAN DHARMA SABHA

**NOTICE OF EXTRA ORDINARY GENERAL MEETINGS**

**An extra ordinary general meeting shall be held on Sunday, 3rd October 2021 at Shree Laxminarayan Mandir at 10:00am - Pramukh Swami Sabha Grah. All members of Tanzania hindu community are required to attend on time.**

The Agenda of the meeting shall be Introduction of the draft of new constitution for Shree Sanatan Dharma Sabha.

After the meeting of 3rd October the members shall be able to read the draft of new constitution at the office of SSDS. And Members should send their questions in writing to the office of SSDS for the attention of the Secretary General after reading the draft and before the review meeting.

A second Extra Ordinary meeting shall be held on 17th October, 2021, Sunday at Shree Laxminarayan Mandir at 10:00am – Pramukh Swami Sabha Grah. All members of Tanzania hindu community are required to attend on time.

**The Agenda of this second meeting shall be as below:**

1. To review and respond to only the questions received by the secretary general of SSDS after reading of the draft of new constitution by the members.

2. To set a date for an Extra Ordinary General Meeting to approve and adopt the draft of new constitution for Shree Sanatan Dharma Sabha.

**Yash Desai**
**Hon. General Secretary**
**Shree Sanatan Dharma Sabha**

*Providing Unity and Religious Leadership to the Hindu Community of Tanzania*

| Shree Sanatan Dharma Sabha | Telephone: | Society Registration No: | E-mail: | Web page: |
|---|---|---|---|---|
| Pramukh Swami Street | +255 22 2132835 | 463 | mandir@ssds.or.tz | www.ssds.or.tz |
| P. O. Box 5 | Mobile: | TIN: | | |
| Dar es Salaam, Tanzania | +255 | 101-321-207 | | |

A member of The Hindu Council of Tanzania


# 'Kimbunga cha Samia' chatikisa TANESCO

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan amerejea nchini akitokea Marekani na kufanya uteuzi wa viongozi mbalimbali, akiwaondoa 'vigogo' wa Shirika la Umeme (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Baada ya kutua kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam jana mchana, Rais Samia alilakiwa na wananchi waliobeba mabango yenye ujumbe wa kumpongeza kwa aliyoyafanya akiwa Marekani alikokwenda kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Muda mfupi baada ya kuwasili nchini, Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari ikibainisha kuwa Rais Samia amemteua Omari Issa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO. Kabla ya uteuzi huo, Issa alikuwa Mtendaji Mkuu wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi (PDB)

Taarifa hiyo ya Ikulu ilibainisha kuwa Rais Samia amemteua Maharage Chande kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO. Kabla ya uteuzi huo, Chande alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kanda ya Afrika Mashariki na Magharibi wa Multichoice Afrika na anachukua nafasi ya Dk. Tito Mwinuka.

Rais Samia pia amemteua Michael Minja kuwa Kamishna wa Petrol na Gesi, Wizara ya Nishati. Kabla ya uteuzi huo, Minja alikuwa Mkurugenzi Mkuu – TIPPER.

Taarifa hiyo ya Ikulu pia ilibainisha Mkuu wa Nchi amemteua Felschemi Mramba kuwa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu. Kabla ya uteuzi huo, Mramba alikuwa Mshauri Mkuu wa Kiufundi – TANESCO Training School.

Pia amemteua Hassan Said kuwa Mkurugenzi Mkuu wa REA. Kabla ya uteuzi huo, Seif alikuwa Meneja wa Kanda Mwandamizi wa Kanda ya Mashariki TANESCO. Said anachukua nafasi ya Amos Maganga.

Taarifa hiyo ya Ikulu ilibainisha kuwa uteuzi huo ulianza Septemba 23, mwaka huu, lakini haikubainisha sababu za kufanyika kwa mabadiliko hayo ya uongozi.

Katika taarifa hiyo, pia ilibainishwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, amewahamisha watumishi waandamizi watano toka TANESCO kwenda Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambako watapangiwa kazi nyingine.

Watumishi hao ni: Khalid James – Naibu Mkurugenzi Mtendaji Uwekezaji; Raymond Seya – Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usambazaji na Masoko; Isaac Chanje – Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usafirishaji; Nyelu Mwamaja – Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi; na Amos Ndegi – Mwanasheria wa TANESCO.

Mabadiliko hayo ya kiongozi ndani ya mamlaka hizo mbili zinazoshughulikia nishati ya umeme nchini yamefanyika ikiwa ni siku chache baada ya Rais Samia kutengua uteuzi wa Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akimteua Mbunge wa Bumbuli, January Makamba kushika wadhifa huo.

## HABARI KITAIFA

# Waganga wakuu mtegoni

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, amewaweka mtegoni waganga wafawidhi wa hospitali za rufani za mikoa kwa mambo matano.

Amesema atawapima utendaji kazi katika ukusanyaji wa mapato, uwajibikaji, uboreshaji wa huduma, ubunifu na kushughulikia malalamiko ya wagonjwa sambamba na wanavyotekeleza maagizo ya ngazi za juu.

Prof. Makubi alibainisha hayo juzi wakati akifungua mkutano wa waganga wafawidhi wa hospitali za rufani za mikoa na kuwataka kutekeleza majukumu yako kikamilifu.

"Tutakuwa tunawapima jinsi gani mnavyoboresha huduma. Inatakiwa mteja akifika aone kwa jinsi gani huduma zimeboreshwa, masuala la ukusanyaji wa mapato ni vizuri kila mmoja wenu akafikia malengo, lakini pamoja na hayo serikali ingependa kuona kwa namna gani mnashughulikia malalamiko ya wateja wenu," alisema Prof. Makubi.

Aliwataka viongozi hao wa hospitali za mikoa kutekeleza maagizo yanayotolewa na ngazi za juu ikiwamo utoaji wa taarifa.

Katika hatua nyingine, Prof. Makubi alisema serikali imedhamiria kuendelea kuboresha huduma za tiba na kinga ikiwamo kupanua huduma za kibingwa katika hospitali za wilaya.

"Tumedhamiria kuboresha huduma za afya huduma hizo hazikuwapo, hususani kwenye hospitali zetu za wilaya, tunafahamu vituo vya afya vingi vilijengwa, ikiwa ni mkakati wa kuboresha miundombinu," alisema Prof. Makubi

Kwa mujibu wa taarifa ya Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. James Kihologwe, waganga hao wanapaswa kupeleka mipango mikakati yao wizarani sambamba na kuangalia mazingira ya sasa ya ugonjwa wa UVIKO-19 ambao umeibua baadhi ya wataalamu wachache wanaoleta shida kadhaa katika suala la maadili kwa wafanyakazi.

"Hivi karibuni yamejitokeza matukio mengi ya watoa huduma kufanya mambo ambayo ni kinyume na maadili na miiko inayoongoza taaluma ya afya, nanyi katika maeneo yenu ya kazi mna mabaraza ya wataalamu hawa, hivyo hakikisheni yanafanya kazi yake vizuri huku mkiyasimamia ili kuhakikisha maadili ya watoa huduma yanaimarishwa," aliagiza Dk. Kihologwe.



Wafanyabishara wadogo maarufu kama machinga wakifanya biashara kwenye njia ya waenda kwa miguu, katika makutano ya Barabara za Bagamoyo na Sam Nujoma, eneo la Mwenge, mkoani Dar es Salaam jana, kitendo kinasababisha usumbufu kwa wapiti njia. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Corona yaleta shida uchangiaji wa damu

**Na Romana Mallya**

MLIPUKO wa virusi vya corona umetajwa kuwa chanzo cha kupungua kwa idadi ya wachangiaji wa damu na kusababisha uhitaji wake kuwa mkubwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), hasa kwa watoto wenye saratani.

Meneja Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kuthibiti Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Omary Ubuguyu, aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya saratani za watoto ambayo yalitanguliwa na matembezi ya hisani na baadae michezo mbalimbali.

Maadhimisho hayo ambayo yalitawaliwa na ushuhuda wa waliopona ugonjwa huo, yaliandaliwa na Idara ya Watoto kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Tumaini la Maisha na Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili (MUHAS).

Dk. Ubuguyu alisema matatizo makubwa wanayokutana nayo sasa ni kuwapo kwa idadi ndogo ya watu wanaojitokeza katika hospitali mbalimbali kuchangia huduma hiyo.

Alisema kabla ya janga la corona, wachangiaji wengi ambao walikuwa wanawategemea wachangie walitokana na matamasha mbalimbali yaliyokuwa yakiandaliwa na kuwekwa huduma hiyo ya kuchangia damu.

"Kwa kuwa tumepunguza matamasha, tumepunguza sehemu ya wachangiaji wa damu waliokuwa wanajitolea huko, tatizo hili wakati huu wa corona limeongezeka zaidi ndiyo maana tunahamasisha watu wachanje," alisema.

Alitolea mfano maadhimisho hayo ya saratani kwa kueleza kuwa wameshindwa kuita idadi kubwa ya watu kwa kuwa bado nchini inapambana kukabiliana na maambukizo mapya ya virusi vya corona.

Dk. Ubuguyu aliwataka Watanzania wajitokeze katika hospitali mbalimbali kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wagonjwa.

"Kuna jamii za watu wa Asia na madhehebu ya dini, wana jumuiya ambazo kwa pamoja huchangia damu lakini Watanzania wengi hamasa ni ndogo, tunawahamisha wajitoe," alisema.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Saratani na Damu kwa Watoto kutoka MNH, Khadija Mwamtemi, alisema moja ya matatizo wanayokutana nayo wakati wakitoa huduma, ni uhaba wa damu.

"Matibabu ya saratani yanahitaji damu, wito wangu kwa jamii tunaomba wasiwe na hofu kuja kuchangia, ukitoa utakuwa umetoa mchango mkubwa kwa sababu katika kutibu hawa watoto, tunapata changamoto kubwa, kuna saratani nyingine hasa za damu unashindwa kumpa mtoto dawa kwa sababu damu yake ipo chini.

"Mfano chembe sahani zikipungua mtoto anatokwa na damu ili uzipate lazima kuwe na damu, tunaomba tuunge mkono Mpango wa Taifa wa Damu Salama, uhitaji wa damu ni mkubwa, tukizungumzia matumizi ya damu sehemu kubwa inakwenda kwa wanaojifungua na watoto wakiwamo wa saratani," alisema.

Dk. Mwamtemi alitaja vikwazo vingine ni suala la miongozi kwa wagonjwa wa saratani, akifafanua kuwa baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakiwaondoa watoto hospitalini inapofikia hatua ya matibabu kwa mionzi kwa kudhani watakufa.

Kelvin Kashaija, mwanafunzi anayeingia mwaka wa tatu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) akichukua Shahada ya Sanaa katika Elimu, alisema kuwa mwaka 2009 akiwa na umri wa miaka 10, aligundulika kuwa na saratani ya damu.

Alisema ilianza kama uvimbe kichwani na alipopelekwa Muhimbili, waliutoa wakijua ni wa kawaida lakini baadaye uvimbe mwingine ukaota pembeni ya kidonda.

Alisema Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa kushirikiana na daktari wa kigeni ambaye ni miongoni waliopo katika Taasisi ya Tumaini la Maisha, walichukua kinyama na kukiotesha nchini kwao na majibu yakaonyesha ana saratani ya damu.

"Nilianza rasmi matibabu ya saratani mwaka 2010, Ocean Road na baadaye tukahamishiwa Muhimbili, nilikaa wodi ilikuwa inaitwa Ujasiri na Tumaini la Maisha, ugonjwa huu niligunduliwa nikiwa darasa la nne mwishoni, nililazwa mwaka mzima wodini na baadaye nikawa ninahudhuria kliniki mpaka nikapona," alisema.

# Mbaroni tuhuma kuua mke

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi linamshikilia Khatour Said Hamad kwa tuhuma za kumuua mke wake, Zulfat Shaikhan Rashid (23).

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kufanya mauaji hayo Septemba 20, mwaka huu majira ya saa moja asubuhi huko nyumbani kwake Kianga, Wilaya ya Magharib A Unguja.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, mtuhumiwa huyo anadaiwa kufanya mauaji hayo dhidi ya mke mdogo huyo na jeshi hilo linaendelea kumshikilia kwa ajili ya uchunguzi zaidi kabla ya kumfikisha mahakamani.

Alisema jeshi hilo lilipata taarifa za awali za mauaji hayo kutoka kwa mfanyakazi wa ndani wa marehemu aliyetambulika kwa jina la Fatma Ibrahim Hassan (18), ambaye alikuwa anashikiliwa kwa mahojiano.

Alisema katika mahojiano ya mfanyakazi huyo, alidai kuwa Septemba 19, mwaka huu majira ya jioni, Zulfat alitoka na mumewe kwa matembezi na kurudi nyumbani kwao Kianga majira ya saa mbili lakini mumewe aliendа kulala kwa mke wake mkubwa, lakini asubuhi alirejea na kudaiwa kutekeleza mauaji hayo.

Katika siku za karibuni, kumekuwa na matukio mengi ya mauaji na ukatili miongoni mwa wanandoa, huku wataalamu wa saikolojia na ustawi wa jamii wakieleza kuwa yanachochewa na vijana wengi kuingia katika uhusiano pasi na maandalizi ya kina.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA MOSHI**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI**
**SHAURI NAMBARI 13 LA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**

**BERNALD ARNOLD CHALE............MAREHEMU**

**CHRISTOPHER PAUL CHALE............MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo ua kabla ya tarehe 2 mwezi wa Desemba, mwaka 2021.

**Imewasilishwa Moshi leo tarehe 20 Mwezi wa Septemba, Mwaka 2021**

RIPOTI MAALUM -2

## MIMBA SHULENI

# Ofisa: Elimu Bure ni tatizo kwa wazazi

## ■Wadau wavinyooshea kidole 'vigodoro'

**Na Elizabeth Zaya**

**KATIKA sehemu ya kwanza wiki iliyopita, kuliainishwa namna mabinti wanavyojiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi katika umri mdogo na mazingira yake yanayochochea mimba shuleni. Endelea kufuatilia uchambuzi zaidi wa hoja hiyo na zingine zinazogusa dosari hiyo ya kijamii:**



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo.

KAIMU Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mtambani iliyoko Kata ya Mapinga wilayani Bagamoyo, Stella Lyimo, anarejea uzoefu wake wa zaidi ya miaka 10 wilayani humo, akilalamika kuwa mwamko kuhusu umuhimu wa elimu ni mdogo katika jamii anayoishi.

"Yaani wazazi wa huku mtoto hata asipoenda shuleni wiki nzima wala hawajali na ukienda kumripoti mtoto kwao kwamba ni mtoro, kibao kinakugeukia wewe, anakuchukia kabisa na kukurushia maneno makali. Bado hakuna mwamko wa elimu, wazazi hawajali kabisa masuala hayo," analalamika.

Mwalimu Stella pia ananyoshea kidole watoto kushiriki ngoma za jadi, maarufu vigodoro, pamoja na hali duni kimaisha inayowakabili wazazi, kuwa ni sehemu ya kiini cha mimba miongoni mwa wanafunzi.

"Wazazi wanaenda na watoto wao kwenye vigodoro, wanacheza na kuwafundisha huko michezo ya kutisha ambayo hawapaswi kujifunza, lakini shuleni hawana muda huo wa kuwasisitiza waende, bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwa wazazi kuhusu malezi bora ya watoto huku kwetu.

"Wazazi wanalala chumba kimoja na mtoto ambaye anajielewa lakini wala hawajali kwamba kuna mambo mengine ni ya hatari kwake ambayo atajifunza kutokana na umri wake, na ndiyo maana inapokuja kwenye suala la elimu wanatupa tabu sisi walimu."

### USTAWI WA JAMII

Ofisa Ustawi wa Jamii Kata ya Kerege, Hawa Iddy, anafungamana na Mwalimu Mkuu Stella, akikiri jamii anayoitumikia bado iko nyuma katika kuhakikisha kunakuwa na malezi bora kwa watoto.

"Malezi kwa watoto huku ni tatizo ambalo tunapambana na wazazi, yaani malezi bora kwa watoto wao siyo kipaumbele kabisa, unakuta wazazi kila mmoja anaondoka nyumbani na kurudi usiku bila kujali watoto wao watakula nini.

"Watoto wengi huku wanajilea wenyewe na ndiyo maana hata hawajali kama wanakwenda shuleni au hawaendi, suala la elimu kwao hawalipi kipaumbele kabisa.

"Tunafanya vikao nao kila mara kuwaelezea hayo mambo yote lakini bado hawabadiliki. Na ndio maana huku ni rahisi sana mtoto kuacha shule au kubebeshwa mimba kwa sababu wakati mwingine wanapokosa mahitaji na wazazi hawajali, watoto wanaamua kujiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi," analalamika.

Katika hilo, Hawa ana angalizo kwa serikali kwamba kuna haja kuangalia namna ya kuboresha sheria ili iwabane wazazi wazembe katika kulea na kutunza familia zao.

"Yaani kama adhabu inavyotolewa kwa wengine wanaowapa ujauzito wanafunzi, ni vyema na hawa wazazi wa namna hii nao wapewe adhabu kali, pengine itasaidia kuwabadilisha," anashauri ofisa huyo.

Taasisi ya Ukombozi inayojishughulisha na utetezi wa haki za watoto wilayani Bagamoyo inabainisha namna inavyochukua jukumu la wazazi kusaidia baadhi ya wanafunzi wanaokatisha masomo yao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mimba za utotoni.

Jumanne Waziri, mmoja wa maofisa wa taasisi hiyo, anataja mikakati yao kuwa inajumuisha kuwatafutia vituo vya kurudia mitihani na inawalipia ada ya mtihani husika.

Hata hivyo, ofisa huyo hayuko nyuma kuumulika mwamko wa wazazi kuhusu elimu, akibainisha kuwa wamekuwa wakikumbana na upinzani mkali kutoka kwa baadhi ya wazazi.

"Tunapojiridhisha kuna mwanafunzi amepata ujauzito katika mazingira ambayo labda ni kutokana na hali ya umaskini, huwa tunazungumza naye na kumshauri anapojifungua afanye hata QT (Mtihani wa Maarifa).

"Cha kusikitisha wakati mwingine tunapofanya hivi tunakumbana na vikwazo sana, wapo baadhi ya wazazi ambao hawataki kabisa watoto wao waende shule, hasa wa kike, na wengine wanakuwa wanawafundisha watoto wasifanye vizuri kwenye mitihani.

"Ninakumbuka kuna mmoja tulimsaidia kumrudisha shuleni, lakini mwisho wa siku alituambia hawezi kuendelea tena na wakati huo tayari tulikuwa tumemlipia ada na kila kitu. Kufuatilia vizuri, wazazi wako nyuma yake.

"Jambo hili lilitushangaza, majibu tuliyokuwa tukipewa na wazazi tulibaini kwamba mtoto amekataa shule kwa shinikizo la mzazi, tutaendelea kuilaumu serikali bure, kumbe wakati mwingine wazazi ndiyo wenye shida," Jumanne anahitimisha.

### KUTOKA HALMASHAURI

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Bagamaoyo, Alois Kaziyareli, katika mazungumzo na Nipashe Jumapili, anabainisha kuwa tangu serikali ianze kutekeleza mpango wa utoaji wa elimumsingi bila ada takribani miaka mitano sasa, wazazi wengi wamesahau majukumu yao ya msingi kwa watoto wao.

"Wazazi wengi wanafikiri kila kitu kwa watoto kinagharamiwa na serikali, mtoto anafika shuleni, hana hata pesa kidogo ya kununulia chakula na wakati mwingine anaona wenzake wanakula, hili ni tatizo.

"Kuna watoto wanaoishi mbali na maeneo ya shule, wanatakiwa wawe na nauli ya kuwafikisha shuleni na kuwarudisha nyumbani, lakini hawapewi, fedha ya chakula hawapewi.

"Wengine wamepanga mitaani kwa sababu wanakotoka ni mbali, kwa hiyo wakati mwingine wanaishiwa chakula na wakikifuata nyumbani mpaka waje wapewe na warudi tena shuleni inawachukua muda mrefu na ndiyo maana wengine huwa wakikumbana na vishawishi wanaharibikiwa kwa sababu hizo.

"Na wapo watoto wengine wanapokwenda kufuata chakula nyumbani, wanachukua muda mrefu, kwa hiyo wanaamua kutulia hawaji shuleni, hizo zote ni kesi tunazokumbana nazo kwa wanafunzi.

"Mimba nyingi nazo zinasababishwa na changamoto hizi wanazopata wanafunzi, ambazo msingi mkubwa ni wazazi wao kushindwa kuwajibika," anafafanua.

Katika kukabiliana na vikwazo hivyo vya kijamii, Ofisa Elimu huyo anasema ofisi yake kwa kushirikiana na maofisa wa Idara ya Ustawi wa Jamii imekuwa ikiitisha vikao vya wazazi shuleni kwa lengo la kukumbushana wajibu, ikiwamo kuchangia utolewaji wa huduma ya chakula shuleni kwa ajili ya maendeleo ya watoto wao.

### MIMBA 130 MWAKA MMOJA

Mwanzoni mwa mwaka huu, akizungumza kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Pwani, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Evarist Ndikilo, alibainisha kuwa kwa mwaka jana, jumla ya wanafunzi 139 walipata ujauzito mkoani humo.

Katika ufafanuzi wake, kiongozi huyo wa mkoa alibainisha kuwa kati ya wanafunzi walioingia katika majukumu ya uzazi ututoni, wa shule za msingi walikuwa 39 na wa sekondari walikuwa 100.

Hivi karibuni serikali kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, ilitangaza kuwaruhusu wanafunzi waliokatisha masomo yao kwa sababu mbalimbali ikiwamo za ujauzito, kurejea masomoni kupitia vyuo vya maendeleo ya wananchi.

Dk. Akwilapo aliwataka wakuu wa vyuo hivyo kutekeleza agizo hilo la kudahili wanafunzi hao ifikapo mwaka 2022 huku akiagiza vituo hivyo visajiliwe kuwa vya kufanyia mitihani ya kitaifa ya kidato cha pili na nne.

Ripoti iliyotolewa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mwaka 2020, ilibainisha kuwa tatizo la wanafunzi kukatisha masomo katika shule za sekondari lipo zaidi katika madarasa ya chini na kwamba kwa kidato cha pili waliokatisha masomo mwaka huo walikuwa asilimia 39.6.

Ilifafanuliwa zaidi katika ripoti hiyo kwamba sababu kuu za wanafunzi kukatisha masomo ni utoro ambao ulikuwa wa asilimia 91.6, ukifuatwa na mimba asilimia 5.5 na vifo asilimia 0.7.

MAKALA MAALUM

Na Esther Mgidula

MIAKA 22 iliyopita Tanzania iliweka mkakati wa kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, lakini azma hiyo ilifikiwa mwaka jana, yaani miaka mitano kabla ya ukomo uliokuwa umewekwa.

Mnamo Juni 1999, serikali ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambayo pamoja na mambo mengine, inalenga kupunguza nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wawe katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Hata hivyo, licha ya Tanzania kuingia katika uchumi wa kati, bado nchi inakabiliwa na vikwazo kadhaa, ukiwamo uhaba wa watumishi serikalini.

Siku tatu zilizopita, Rais Samia Suluhu Hassan akiwa jijini New York, Marekani, alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya (EU), Charles Michel na kukiri nchi kukabiliana na uhaba wa watumishi katika baadhi ya sekta.

Katika mazungumzo yao hayo, Michel alimshukuru Rais Samia kwa kukutana naye na kueleza kuwa lengo lake ni kutaka kupata maoni ya Mkuu wa Nchi huyo kuhusu mambo manne ya kipaumbele kwa Umoja wa Ulaya kwenye uhusiano wake na Afrika na utayari wa Umoja wa Ulaya kushirikiana na Tanzania kwenye maeneo hayo.

Mambo hayo ni UVIKO-19, Mabadiliko ya Tabia Nchi, Hali ya Usalama Msumbiji na Mapinduzi ya Kidijitali.

Rais Samia aliushukuru Umoja wa Ulaya kwa ushirikiano wake na kuelezea hatua ambazo Tanzania inachukua katika kukabiliana na UVIKO-19, hasa ikizingatiwa kuwa ugonjwa huo umeathiri sekta nyingi ikiwamo ya utalii.

Pamoja na mambo mengine, Rais Samia alieleza hatua mbalimbali ambazo serikali inachukua katika kusambaza miundombinu ya afya ingawa bado kuna vikwazo katika upatikanaji wa vifaa tiba na rasilimali watu na hivyo kuukaribisha Umoja wa Ulaya kuangalia namna ya kushirikiana na Tanzania katika maeneo hayo.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hayuko mbali katika kuumulika uhaba wa watumishi serikalini na madhara yake.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu, anabainisha kuwa amebaini kuna uhaba wa watumishi takribani 120,000 (takwimu hali 119,753) katika mamlaka za serikali za mitaa alizozikagua.

"Mapitio ya ikama za mamlaka 123 za serikali za mitaa yalibaini idadi halisi ya watumishi waliopo ni 233,281 kulinganishwa na mahitaji ya watumishi 353,034 na kusababisha upungufu wa watumishi 119,753, sawa na asilimia 34 ya idadi inayohitajika.

"Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa mamlaka za serikali za mitaa ikiwa pamoja na utoaji



Kaimu Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora, Donald Rweramila.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi.

# Uhaba wa watumishi; dosari nyingine kiutendaji serikalini

## ■CAG abaini upungufu watumishi 120,000, ahadharisha huduma duni
## ■Chuo chapata suluhisho kitaalamu

duni wa huduma, mrundikano wa majukumu na kupunguza morali ya kazi kwa watumishi waliopo.

"Pia, nilibaini kuwa malengo ya serikali ya kutekeleza miradi mingi kwa kutumia utaratibu wa nguvukazi ambayo inahitaji wataalamu wa kutosha katika mamlaka za serikali za mitaa yanaweza yasifikiwe kwa mafanikio kutokana na upungufu huu wa watumishi," CAG Charles Kichere anahadharisha.

Wakati CAG akitoa angalizo hilo, Nipashe Jumapili inabaini uhaba wa watumishi hauko kwenye mamlaka za serikali za mitaa pekee, bali maeneo mengine, zikiwamo baadhi ya wizara.

Katika hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka huu wa fedha aliyoiwasilisha bungeni Mei mwaka huu, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alibainisha kuwa wizara hiyo inakabiliwa na naksi ya watumishi 3,114.

Lukuvi alifafanua kikwazo hicho cha kiutendaji, akibainisha: "Kwa sasa, wizara ina jumla ya watumishi 2,378. Kati yao, watumishi wa kada za Sekta ya Ardhi ni 1,733.

"Ili wizara iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, inapaswa kuwa na watumishi wa kada za Sekta ya Ardhi wapatao 4,847. Hivyo, wizara ina upungufu wa watumishi 3,114 wa kada za Sekta ya Ardhi."

Katika kusaka dawa ya tatizo hilo, uongozi wa Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) unasema kimepiga hatua kubwa ikiwamo kuongeza idadi ya wanafunzi ili kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa ardhi nchini.

Unabainisha kuwa katika mpango kabambe wa miaka 10 (2010-2020) kimeongeza udahili mwaka hadi mwaka, idadi ya wanafunzi ikiongezeka kutoka wanafunzi 146 mwaka wa masomo 2009/10 hadi kufikia 1,414 mwaka 2020/21.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Donald Rweramila, anasema kuwa tangu kilipoanzishwa mwaka 1979, kilikuwa kikiongeza udahili wa wanachuo kulingana na miundombinu iliyokuwapo. Anabainisha kuwa mwaka 2009, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilibuni mpango kabambe wa miaka 10 uliolenga kupanua chuo hicho kwa kuongeza miundombinu, kuongeza vitendea kazi ambavyo vilileta ongezeko la idadi ya wanachuo kutoka 146 mwaka 2009/10 hadi 1,414 mwaka 2020/21.

Kiongozi huyo anasema chuo kimefanikiwa kuandaa na kuboresha mitaala yote kwa kufuata mfumo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ili tuzo zitolewazo na chuo hicho ziwe na kiwango cha ubora unaokubalika kitaifa na kimataifa.

Kiongozi huyo anasema fani hizo ni muhimu hasa katika uwekezaji mkubwa wa viwanda ambao Tanzania inafanya kwa mafanikio makubwa kwa lengo la kuimarisha uchumi wa nchi na kutoa ajira kwa raia wake. Anasema wamefanikiwa kupata usajili na ithibati kamili kutoka NACTE ya kutoa mafunzo ya Sekta ya Ardhi katika ngazi ya astashahada na stashahada.

"Wahitimu katika ngazi ya stashahada wenye ufaulu stahiki wanazo sifa za kujiunga na masomo ya shahada ya kwanza katika chuo kikuu chochote ndani na nje ya nchi kinachofundisha taaluma za Sekta ya Ardhi au zinazohusiana," anasema.

Anaongeza kuwa chuo pia kimeboresha mfumo wa upatikanaji wa maji safi kwa matumizi ya wanachuo katika bweni jipya kwa kujenga tanki la kuhifadhi maji chini ya ardhi lenye ujezo wa lita 200,000.

Chuo hicho pia kimeboresha mfumo wa umeme kwa kuingiza umeme wa njia tatu na kusimika transfoma ndani ya eneo la chuo ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la matumizi ya umeme," alisema na kubainisha kuwa wamenunua jenereta kubwa lenye uwezo wa kuhudumia eneo lote la chuo wakati wa upungufu au hitilafu ya umeme unaotolewa na Shirika la Umeme (TANESCO).

Anasema chuo hicho pia kimefanikiwa kuanza ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua watumiaji 360 na kompyuta 50 kwa wakati mmoja.

"Chuo kimefanikiwa kusimika Mfumo wa udahili wa Wanafunzi ambao umebuniwa na kusimikwa na Chuo Kikuu Ardhi – Dar es Salaam.

"Mfumo huu shirikishi unasaidia kurahisisha usajili wa wanachuo, kutunza kumbukunbu sahihi za wanachuo, utangazaji wa matokeo ya mitihani na kudhibiti ulipaji wa ada za masomo kwa wanachuo," anasema.

Anabainisha chuo kimefanikiwa kuendelea kufanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali iliyopo chuoni ikiwa ni pamoja na ofisi za watumishi, madarasa, mabweni ya wanachuo na unuzi wa samani.

Tangu chuo kilipoanzishwa mwaka 1979 hadi mwaka 2017, kimefanikiwa kutoa jumla ya wahitimu 3,303.

Chuo hicho kilianzishwa mwaka 1979, kikiwa ni zao la kilichokuwa Kituo cha Mafunzo ya Ndani ya Urasimu Ramani (Map Draughtsmanship) kilichoanzishwa mwaka 1955, kilichokuwa na makao makuu Dar es Salaam.

Rweramila anakumbusha kuwa mnamo Julai 1964, serikali iliboresha mitaala na kuongeza muda wa mafunzo hadi kufikia miezi sita. Mwaka 1979, wizara ililazimika kutafuta eneo jingine kwa ajili ya kupanua mafunzo hayo kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya wataalamu wa urasimu ramani.

Kutokana na hali hiyo, wizara iliamua kuhamisha eneo la mafunzo na kuyapeleka mkoani Tabora katika majengo ya muda yaliyoachwa na Kampuni ya upimaji iliyojulikana kwa jina la 'Kenting Surveys' kutoka Canada.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua ya Rais Samia kuifagia TANESCO ni ya kupongezwa

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, jana alitangaza kufanya uteuzi wa viongozi mbalimbali lakini kubwa zaidi ameligusa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) baada ya kufagia menejimenti nzima pamoja na kumwondoa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Dk. Alexander Kyaruzi.

Katika mabadiliko hayo, Rais ametengua uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dk. Tito Mwinuka na kumteua Maharage Chande kushika nafasi hiyo. Kabla ya hapo, Chande alikuwa Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Magharibi wa MultiChoice Africa. Nafasi ya Dk. Kyaruzi imechukuliwa na Omari Mussa, aliyekuwa Mtendaji Mkuu Kitengo cha Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi (PDB).

Licha ya mabadiliko hayo, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, amewahamisha watumishi waandamizi watano wa TANESCO kwenda Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambako watapangiwa kazi nyingine.

Waliohamishwa na vyeo vyao kwenye mabano ni Mhandisi Khalid James (Naibu Mkurugenzi Mtendaji Uwekezaji), Mhandisi Raymond Seya (Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usambazaji na Masoko), Mhandisi Isaac Chanji (Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usafirishaji), Nyelu Mwamaja (Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi) na Amos Ndegi (Mwanasheria wa TANESCO).

Mabadiliko hayo pia yamegusa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kumpata Mkurugenzi Mkuu mpya wa taasisi hiyo ambaye ni Hassan Seif Said anayechukua nafasi ya Amos Maganga.

Wako wengine ambao wameteuliwa kuwa makamishna katika Wizara ya Nishati lakini kilichotikisa ni mabadiliko ndani ya taasisi hizo zilizopewa dhamana ya kuhakikisha umeme unapatikana mijini na vijijini ili kufikia ndoto ya kweli ya kuwa na Tanzania ya viwanda.

Kupanguliwa kwa safu ya uongozi ndani ya TENESCO na REA kumefanyika ikiwa ni takriban wiki mbili tangu aliyekuwa Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kuondolewa katika nafasi hiyo kutokana na mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri.

Hatua hiyo ya Rais Samia kuwaondoa viongozi hao pia imechukuliwa kukiwa na malalamiko makubwa ya kiutendaji kwenye sekta ya nishati. Moja ya malalamiko hayo ni kukatika kwa umeme mara kwa mare tena bila taarifa za msingi huku baadhi ya maofisa wake wakijitetea kuwa wanabadilisha nguzo kwa kuondoa zile za miti na kuweka za sementi.


Licha ya umeme kukatika, pia kumekuwa na urasimu kwa wateja ambao wamekuwa wakiomba kufungiwa umeme kwenye maeneo yao. Baadhi ya wateja wamekuwa wakilalamika kuwa wanasubirishwa kwa zaidi ya miezi mitatu ndipo wapate huduma huku yakiwekwa mazingira ya rushwa na baadhi ya maofisa wa shirika hilo.

Pia kwa upande wa REA, wananchi maeneo ya vijijini wamekuwa wakilalamika kushindwa kupatiwa huduma hiyo na wakati mwingine makandarasi waliopewa kazi za kupeleka umeme wakishindwa kutekeleza kazi hiyo kama ilivyoainishwa katika mikataba.

Kutokana na mabadiliko hayo, ni imani ya Watanzania kuwa uongozi mpya katika taasisi hizo nyeti utachukua hatua za haraka kurekebisha kasoro zilizokuwa zinalalamikiwa juu ya urasimu wa kupatiwa huduma na kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Pamoja na kwamba ni matumaini viongozi hao wapya watafanya hivyo, wanayo kazi kubwa kuonyesha kwa vitendo kwamba wameaminiwa na Rais katika kutekeleza majukumu hayo na kukata kiu ya Watanzania juu ya upatikanaji usioridhisha wa nishati hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kunani miradi ya maendeleo kususiwa na Mwenge wa Uhuru?

**MWENGE** wa Uhuru hukimbizwa mikoa yote nchini kila mwaka, huku mbio hizo zikiambatana na uzinduzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotekelezwa na serikali kwa kushirikiana na wadau wake.

Hata hivyo, katika mbio hizo, kila mwaka yamekuwa yakijirudia makosa ambayo ni ujenzi wa miradi chini ya kiwango na kusababisha viongozi wa mbio hizo kukataa kuizindua.

Ninaamini kuwa viongozi hao wanachukua hatua hiyo kwani miradi kuwa chini ya kiwango na kutoendana na gharama halisi ni sawa na kukwamisha maendeleo ya wananchi wa maeneo husika na taifa kwa ujumla.

Kwa mfano, mwaka 2019, aliyekuwa kiongozi wa mbio hizo, Mzee Mkongea, alikataa kuzindua miradi miwili ya maji na barabara Wilaya ya Tarime mkoani Mara kutokana na kutokidhi vigezo.

Akagusia mradi wa maji wa mtaa wa Gamasara wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 484.9 kwamba ulikuwa na kasoro nyingi ikiwamo nondo zilizotumika katika ujenzi huo kutopimwa kitaalam.

Kwa ujumla ni kwamba kuna baadhi ya miradi katika maeneo mbalimbali ya nchi haikuzinduliwa kwa mwaka huo wa 2019 na ndivyo imekuwa ikitokea kila mwaka wakati wa mbio za mwenge huo. Bahati mbaya mwaka jana hakukuwa mbio za mwenge kutokana na janga la corona na inawezekana kama zingekuwapo, ninadhani 'madudu' katika miradi ya maendeleo yangeendelea kuibuliwa na kutozinduliwa. Ninahisi hivyo kutokana na kwamba, katika mbio za mwaka huu ambazo sasa zinaelekea ukingoni, kiongozi wake Luteni Josephine Mwambashi, ameshatakaa baadhi ya miradi huku sababu zikiwa ni zile zile za kila mwaka.

Hali hiyo inasababisha kuwapo kwa maswali kwamba, watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao wanakwama wapi kutimiza wajibu wao inavyotakiwa?

Kwa mfano, mwaka huu mwenge ukiwa mkoani Mara, Luteni Mwambashi alikataa kuweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) wilayani Butiama. Alichukua hatua hiyo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo matumizi makubwa ya fedha yasiyoendana na thamani ya majengo, baadhi kujengwa kwa gharama kubwa akitolea mfano banda la walinzi.

Kwamba hadi kukamilika litagharimu Sh. milioni 10 na kufafanua kuwa hadhi ya kibanda hicho hailingani na thamani ya kiasi cha fedha kilichotumika, hivyo akaona hakuna haja ya kuzindua mradi huo.

Si hapo tu, bali akiwa Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, alikataa kuzindua mradi wa maji baada ya kubaini kuwa mradi huo ulikuwa uwe na vituo 16 vya kutolea maji, lakini akabaini kuwapo kwa vituo sita tu vinavyotoa maji.

Hali kama hiyo ya uchakachuaji wa miradi, alikutana nayo kwenye mradi mwingine wa maji katika Kata ya Somanga wilayani Kilwa Mkoa wa Lindi na kuagiza TAKUKURU wilayani humo kufanya uchunguzi.

Taasisi hiyo ilipewa kazi ya kuchunguza Sh. milioni 176 zilizotumika katika mradi huo, kwa kuwa haziendani na mradi uliotekelezwa, ambao ni ujenzi wa tangi la lita 100,000 na nyumba moja ya mitambo.

Kwa ujumla nionavyo ni kwamba kuendelea kuwapo kwa matukio ya kukataa kuzinduliwa kwa baadhi ya miradi ya maendeleo, kuonyesha kuwa huenda wapo baadhi ya watendaji wasiosimamia majukumu yao inavyotakiwa.

Wakati huu ambao mbio za Mwenge wa Uhuru zilizoanza Mei, mwaka huu, zikielekea ukingoni, nadhani kuna haja wale wote waliopewa majukumu ya kusimamia miradi ya maendeleo wakatanguliza uzalendo.

Hatua hiyo inaweza kuleta ufanisi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo imekuwa ikitumia fedha nyingi zikiwamo za walipa kodi na nyingine kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

Miradi kuwa chini ya kiwango ni sawa na kukwamisha maendeleo ya wananchi wa maeneo husika na taifa kwa ujumla, hivyo ingependeza kama wasimamizi wakajiuliza wanakwama wapi kuchukua hatua.

Haipendezi kuona kila mwaka baadhi ya miradi ya maendeleo kukwama kutokana na sababu ambazo wakati mwingine zinaweza kuwa ndani ya uwezo wa watu waliopewa jukumu la kuisimamia.

# SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# *Kwa nini Rais apande ndege za watu wengine ilihali tuna zetu?*



Na Pascal Mayalla

**Lakini kipindi cha awamu ya tano chini ya JPM, Tanzania imejenga uwezo sasa tuna ndege kubwa za abiria za masafa marefu. Sasa kwa nini rais wetu aendelee kusafiri na ndege za mashirika mengine wakati sisi tunalo shirika letu la ndege na tunazo ndege za masafa marefu aina ya Boeing, Airbus "The Dreamliner"?**

NAANZA kwa kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwenda Marekani na kulihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA). Japo ziara za nje kwa awamu iliyopita zilionekana kama kupoteza fedha, kiukweli ni nzuri na zenye manufaa hata kama si faida ya papo kwa papo.

Ile Rais wetu kujichanganya na maraisi wenzake, wafanyabiashara na wakurugenzi wa kampuni kubwa za kibiashara, kunaleta manufaa makubwa kwa taifa ikiwamo kuitangaza nchi.

Kwa kawaida Rais akisafiri, huwa tunaonyeshwa picha na video akiwa uwanja wa ndege siku akiondoka huku akionekana anapanda ndege na siku akirudi pia tunaonyeshwa akishuka kwenye ndege na kuandaliwa mkutano na waandishi wa habari uwanjani hapo na kutujuza kilichojiri huko.

Safari hii ya Mama Samia kwenda UN, hatukuonyeshwa akipanda ndege bali tulionyeshwa amefika Marekani akijichanganya na Watanzania, akiwamo Mtanzania mwenzetu maarufu aishie huko, mange Kimambi au Da Mange kama baadhi walivyozoea kumwita.

Hakuna chombo cha habari kinachojiuliza kwa nini Rais amesafiri kimya kimya, apokewe kimya kimya na kuibuka tu. Enzi za Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa na awamu ya nne, Jakaya Kikwete, wakati wa safari za mbali, vyombo vya habari tulialikwa kumsindikiza na alikuwa anaandamana na kundi kubwa la wafanyabiashara. Enzi hizo pia Rais wetu alipanda ndege za mashirika mengine kwa sababu wakati huo, Tanzania tulikuwa hatuna ndege zenye uwezo huo.

Lakini kipindi cha awamu ya tano chini ya JPM, Tanzania imejenga uwezo sasa tuna ndege kubwa za abiria za masafa marefu. Sasa kwa nini rais wetu aendelee kusafiri na ndege za mashirika mengine wakati sisi tunalo shirika letu la ndege na tunazo ndege za masafa marefu aina ya Boeing, Airbus "The Dreamliner"?

Enzi za Magufuli pale Ikulu, nilipopata nafasi, kabla ya kuuliza swali, nilitoa hoja ya waandishi tushirikishwe kwenye mambo ya kuitangaza vizuri nchi yetu na nikasema waandishi tutajitegemea kwa usafiri chakula na malazi. Nimesafiri sana na Mkapa na JK, hivyo hii sasa ni zamu ya Samia, akisafiri safari za kimataifa, itolewe fursa kwa vyombo binafsi na wafanyabiashara kuandamana na rais.

Bila hata kusubiri majibu ya serikali au ya ATCL, sababu pekee iliyomfanya Rais Samia kusafiri kwenda Marekani kwa ndege za abiria za mashirika mengine ni kwanza ATCL haina ruti ya Marekani. Pili, kupeleka ndege kubwa kama Dreamliner Marekani ni gharama. Mafuta na tozo za kutua na kukaa uwanjani zinalipwa kwa saa, hivyo kutumia ndege za mashirika mengine ya kibiashara ni nafuu.

Kama ilivyo katika kutangaza utalii, kuandaa filamu ya utalii na kuitangaza katika vyombo vya kimataifa ni ghali, lakini kama tunataka kukuza utalii, hatuwezi kuepuka gharama, ndiyo maana tumekubali rais wetu kurekodi filamu ya Royal Tour kuutangaza utalii wetu. Hakuna kitu kinachoongoza kuvutia utalii kama usafiri wa ndege za moja kwa moja. Hakuna kitu kingeitangaza Tanzania Marekani kama ndege ya ATCL kutua uwanja wa ndege wa Kimataifa wa JFK, New York, Marekani ikiwa imembeba Rais wa Tanzania.

Rais wa Tanzania kwenda nchi yoyote ikiwamo Marekani kwa ndege ya watu wengine, wakati ATCL inazo hizo ndege ni kosa. Kosa sio kufanya kosa, kosa ni kurudia kosa. muda wowote mwakani, kuanzia miezi ya mwanzoni, Rais atakuwa na ziara Marekani ambayo pia ataizindua rasmi filamu ya Royal Tour. Naomba sana, tusifanye tena kosa la kurudia kosa kwa Rais kutua Marekani kwa ndege za watu wakati tunazo ndege zenye uwezo wa kuruka na kufika huko.

Kitu cha kufanyika ni baada ya kujua filamu ya Royal Tour inayomwonyesha 'movie star' wa Tanzania, Chifu Hangaya itazinduliwa lini Marekani, tujue Dreamliner inabeba abiria 300, ukiondoa Rais na ujumbe wake wa serikali. Kwanza, serikali inatangaza fursa kwa taasisi zote za umma, wenye mambo yoyote ya kufanya Marekani, wapange zifanyike kipindi hicho. Wa serikali hao wafanye 'booking' ATCL na baada ya hapo ATCL inatangaza punguzo la nauli kwa safari ya Marekani inayodumu siku saba.

Hivyo Taarifa tu kuwa Rais wa Tanzania ametua Marekani na dege la Tanzania, akiandamana na ujumbe wa watu 300, ni tangazo tosha la utalii kimataifa. Hakuna ndege yoyote ya moja kwa moja kutoka Marekani hadi Tanzania, hivyo ATCL pia itapata fursa ya kuanzisha ruti ya Marekani na ndege itajaa.

**pascomayalla@gmail.com**
**0754 270403**

**Sababu pekee iliyomfanya Rais Samia kusafiri kwenda Marekani kwa ndege za abiria za mashirika mengine ni kwanza ATCL haina ruti ya Marekani.**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# *Kijaji karibu kwenye tasnia ya habari*



Na Joseph Kulangwa

**Mwalimu alichukiwa na kupachikwa jina ambalo sitalitaja hapa. Si kwamba alichukiwa na darasa lote, la hasha, kuna waliokuwa wakiliweza somo hilo na kuwa marafiki zake, lakini kina sisi tuliomchukia, tulijikuta hata somo tumelichukia na kushindwa kulielewa.**

SAIKOLOJIA ni taaluma muhimu sana katika kutambua tabia ya mtu. Husaidia sana walimu kutambua na kuwajua wanafunzi wao katika mchakato wa kutoa na kupokea mafunzo.

Walimu wasiojua kuitumia vyema taaluma hiyo, hujikuta katika matatizo makubwa, yakiwamo ya kuchukiwa na hata kususiwa na wanafunzi, lakini pia ugumu katika utoaji elimu kwa walengwa.

Nakumbuka tulivyokuwa tukimchukia mwalimu wetu wa Hesabu tukiwa katika madarasa ya chini. Mwalimu ambaye alikuwa na tabia ya kuingia darasani na kiboko mkononi na kuuliza maswali yanayohitaji majibu ya papo kwa hapo.

Aliuliza maswali ya kwenye tebo. Kila aliyekosa kujibu vizuri alichapwa. Hali hiyo ilifanya wanafunzi kuchukia somo lake na wengi kuhofia kukaa madawati ya mbele ambako mara nyingi alianzia kuuliza maswali yake.

Mwalimu alichukiwa na kupachikwa jina ambalo sitalitaja hapa. Si kwamba alichukiwa na darasa lote, la hasha, kuna waliokuwa wakiliweza somo hilo na kuwa marafiki zake, lakini kina sisi tuliomchukia, tulijikuta hata somo tumelichukia na kushindwa kulielewa.

Ufundishaji una mbinu zake na hasa kama wanaofundishwa ni watoto, bila kuwaingizia vivutio fulani hivi wanaweza wasielewe kitu na kama mwalimu atakuwa ni wa kiboko mkononi kila mara, watamwogopa na kubaki manunda tu.

Mwalimu wetu huyo wa Hesabu tulikuwa tunahofia hata kumwuliza swali pale hesabu zilipotushinda. Tulipomfuata alitubamiza na kutusimanga kuwa tuna vichwa vizito visivyoelewa, hivyo kubaki gizani.

Waziri mpya wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, ameingia wizarani kama mwalimu mkali ambaye tayari ameshawaona wanafunzi wake wana makosa, hivyo kuwatishia kwa fimbo kwamba hajafika kucheza bali kuhakikisha manunda wanaonja joto ya jiwe.

Kuanza na onyo kuwa serikali haitavumilia vyombo vitakavyoandika habari zinazohatarisha usalama wa nchi au kusababisha mtafaruku ni sawa, lakini hapakuwa mahali pake kwa sababu inaonyesha tayari ameingia na fimbo mkononi.

Si kweli kwamba vyombo vya habari vina lengo ovu kwa jamii au taifa, la hasha. Nia na lengo lao ni kuhakikisha amani na utulivu vinatamalaki katika jamii, kupitia habari zao zinazotangazwa au kuandikwa.

Ni dhahiri kuna makosa katika uandishi na utangazaji, lakini mengi kwa kiasi kikubwa husababishwa na makosa ya kibinadamu, kama zilivyo ajali za barabarani na kwingineko, hakuna mtu anayefanya makusudi kuchafua au kuhatarisha usalama wa nchi.

Bila shaka Waziri Kijaji kuingia wizarani akiwa amejihami tayari, kunasababisha hata wanahabari nao kujihami kwamba huenda wakati wowote fimbo itawaangukia na matokeo yake ni kufanya kazi bila kujiamini na hatimaye kuharibu.

Simfundishi kazi ila nazingatia ushauri wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kukosoana na kushauriana kwa staha. Alichotakiwa kufanya Waziri wetu ni kubisha hodi wizarani kama alivyofanya, akazungumza na watumishi kama alivyofanya na kisha kuonana na wadau.

Wadau kwa maana hiyo ni pamoja na wanahabari ambao bila shaka angebadilishana nao walichonacho na alichonacho. Ni dhahiri kuwa kuna mambo mengi yeye akiwa waziri mpya katika wizara hii, angependa ayajue lakini pia wanahabari wangependa ayajue.

Hali kadhalika naye angependa wanahabari wajue nini anakitaka, nini anataka kumsaidia Rais Samia katika wizara hii ambayo sasa imekuwa mpya, ambayo ungekuwa uwezo wangu, ningeiita Wizara ya Habari na Mawasiliano na kuacha Teknolojia ya Habari ambayo iko katika wizara zote.

Najua kwa uwezo alionao ambao alishauonesha tangu akiwa Wizara ya Fedha na Mipango wa kupanga na kudadavua hoja na kuzijibu. Ni matumaini ya wadau wa habari wengi watafaidika na uongozi wake ambao utalenga kutatua matatizo yaliyopo, lakini kubwa ni kutekeleza maelekezo ya Rais Samia.

Waziri Kijaji anakabidhiwa Wizara kukiwa na vyombo vya habari ambavyo bado viko kifungoni licha ya Rais kuagiza vifunguliwe lakini pia kukiwa na sheria zisizo rafiki kwa tasnia zinazotakiwa sasa kuondolewa kabisa. Vinginevyo mgeni njoo mwenyeji apone na si akome. Karibu Waziri Kijaji.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Rais kukutana na Mange si jambo la ajabu



Na Thobias Mwanakatwe

**Watanzania wenzangu hii dunia hatuendi hivyo. Naomba mtambue kuwa hakuna mahali itakapowezekana marafiki wa Magufuli wawe marafiki wa Rais Samia au maadui wa JPM wawe maadui wa Samia.**

NIANZE kwa kuwasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bila shaka wasomaji wangu wa safu hii huko mliko mtakuwa mumeitika...Kazi Iendelee.

Leo nimeona nizungumzie safari ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Marekani ambayo nimeona imezua mjadala kabla na baada ya rais kuwasili nchini humo.

Septemba 18, mwaka huu, Rais Samia alianza safari ya kwenda New York, nchini Marekani kuhudhuria Mkutano wa 79 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA). Akiwa nchini Marekani Septemba 23, alipata fursa ya kulihutubia baraza hilo.

Rais pia alihudhuria mkutano wa kilele wa kujadili masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi, usalama wa chakula na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG). Kadhalika, alitumia fursa hiyo kukutana na wakuu wa nchi zingine na viongozi wa mashirika ya kimataifa kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na uhusiano baina ya Tanzania na nchi hizo pamoja na mashirika hayo.

Ikumbukwe ziara ya Rais Samia nchini Marekani ni ya kwanza kwenda nje ya Bara la Afrika tangu apishwe kushika wadhifa huo.

Katika safari hiyo ya Rais, kilichozua maswali mengi kwenye mitandao ya kijamii ni baada ya kukutana na mwanadada Mtanzania anayeishi nchini Marekani, Mange Kimambi.

Kwenye mitandao hiyo, nimeona baadhi ya watu wakikasirika sana na kusema kitendo cha Rais kukutana na Mange ni sawa na kuwa amemsaliti aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli. Watanzania wenzangu hii dunia hatuendi hivyo. Naomba mtambue kuwa hakuna mahali itakapowezekana marafiki wa Magufuli wawe marafiki wa Rais Samia au maadui wa JPM wawe maadui wa Samia.

Magufuli alipoingia madarakani hakuwafanya marafiki wa mtangulizi wake Jakaya Kikwete, kuwa marafiki zake wala maadui wa Kikwete hakuwafanya kuwa maadui zake.

Mwanasaikolojia Vivian Okoye aliwahi kusema ni muhimu kuifanya dunia sehemu salama ya kuishi kuliko kuwa 'busy' kurithishana maadui toka kizazi kimoja kwenda kingine.

Pia ifahamike kuwa hakuna mahali duniani inawezekana kuwa unayemchukia watu wote duniani wamchukie mtu huyo huyo. Hata wewe binafsi si wote wanaokupenda na si wote wanaokuchukia.

Aliokuwa anawapenda Kikwete unajua JPM alipoingia madarakani walipoteana? Dunia hii ni mzunguko. JK aliwahi kutuambia "usirithi adui wa mtu na usiwe na uadui na mtu uadui hauna tija. Fanya kazi na kila mtu ili ujue nani ni nani katika maisha yako, lakini akili za kuambiwa changanya na zako."

.Nani anakumbuka suala la Babu Seya? Alifungwa kipindi cha JK, JPM akamfungulia tena kirahisi sana. Hakuna haja ya kurithi maadui. Hakuna kanuni ya aina hiyo duniani kokote kuwa adui yako ni adui yangu. Ni kukosa tu maarifa na utambuzi.

Kwa hiyo wanaoendelea kujadili suala la Rais Samia kukutana na Mange wapoteza muda wao kwani jambo hilo halina mashiko.

Watanzania bila shaka aliyetuloga alishakufa na kaburi lake halijulikani lilipo. Si mara moja unakuta jambo dogo tu linazua mjadala kwenye mitandao ya kijamii hata kama jambo hilo halina maslahi kwa taifa.

Niwaombe mitandao ya kijamii tuitumie vizuri na si kuzua mijadala ambayo haina maslahi kwa taifa.

Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe

**mwanakatwe2015@gmail.com**
**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU MBARIKI RAIS SAMIA SULUHU HASSAN**

## DARASA LA NDOA

# NAFASI YA MAWASILIANO KATIKA KUJENGA NDOA IMARA- 3



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

KATIKA Jumapili mbili zilizopita, tuliona kuwa mawasiliano ni jambo muhimu katika uhusiano na kwamba yanapokosekana athari zake ni nyingi. Hata pale mawasiliano yanapokuwapo, lakini yanapokosa nidhamu na utaratibu, huweza pia kuharibu uhusiano.

Pia tulijadili mambo ya msingi ya kuzingatia katika kuimarisha mawasiliano yakiwamo kujifunza, kutoogopana na kusikiliza na majukumu. Sehemu hii ya mwisho inaendelea na mambo hayo ya msingi yakiwamo majukumu.

Katika majukumu, baada ya kuzaliwa mtoto kumekuwa na tatizo la mawasiliano baina ya wanandoa. Baada ya watoto kuzaliwa, imetokea wanawake wengi kushughulika zaidi na malezi ya watoto kiasi cha kuzorotesha mawasiliano na waume zao. Baadhi ya ndoa zimejikuta uhusiano wao ukianza kuzorota na kupoteza msisimko. Ni busara, mke asiwe katika harakati za kulea watoto kiasi cha kumsahau mume wake. Watoto wanahitaji wazazi ambao wanawasiliana vizuri baina yao.

Badala ya majukumu kuwatenga wanandoa kimawasiliano, inabidi hayo ndiyo yawalete karibu. Ni ndani ya mawasiliano ambapo majadiliano na kushirikiana kihisia kunapoweza kutoa msaada mkubwa kumpunguzia kila mmoja mzigo. Hivyo inabidi wanandoa kupanga muda wa pamoja ambapo kila mmoja atapata nafasi ya kuwasiliana na kushirikishana na mwenzake. Ni hatari sana kwa wanandoa kukosa muda wa pamoja. Kukosa muda wa pamoja, hufifisha pendo.

Imetokea mahali pengine, watu wamefunga ndoa mpya na shughuli zao kuliko wenzi wao. Yaani, mwenzi anathamini shughuli zake zaidi kuliko mawasiliano na mwenzake. Kwa bahati mbaya kwa sehemu kubwa wahusika hapa ni sisi wanaume ingawa katika zama hizi, wako baadhi ya wanawake ambao wana tatizo hili pia. Unakuta mtu anaporudi anakuwa amechoka sana na anachoweza kufanya ni kuoga na kujitupa kitandani, hata kula mara nyingine inaweza kuwa shida. Mwenzake anapojaribu kuzungumza naye, kauli inayotoka ni moja tu, 'Nimechoka, niache nilale.'

Ndoa za namna hii ni lazima ziwe na nyufa nyingi sana, kiasi kwamba ikiguswa kidogo tu kuporomoka ni rahisi sana. Kuna wengine wanadhani fedha au kipato kinaweza kuchukua nafasi ya mke, mume au familia. Itokeapo hivyo, mwenzi huhisi kuwa hapendwi tena, hathaminiwi na hasikilizwi. Mwenzi anakuwa hana mahali pa kupeleka hisia zake, anaona hana mtu wa kumsikiliza kwa lolote.

Ni muhimu wanaume wenzangu wakafahamu kwamba hata siku moja kipato hakiwezi kuchukua nafasi ya umuhimu wa mawasiliano katika ndoa. Mara nyingi wanaume wa aina hii huwa wanajidanganya kwamba baada ya muda fulani watakuwa wametimiza malengo na wataweza kutulia. Lakini ukweli ni kwamba hili haliwezekani, halijawahi kuwezekana na halitakuja kuwezekana hadi siku ya mwisho ya maisha ya hapa duniani.

Ili kuepukana na matatizo ya kutokuwa na mawasiliano, inabidi wanandoa wawe na dhamira ya kuwasiliana na kupanga kwa makusudi kabisa kuwa na muda wa pamoja. Lazima kuwa na utaratibu utakaotoa nafasi ya kutosha ya mawasiliano na mwenzi. Mwanandoa asiyependa kuwasiliana na mwenzi wake atakuwa anatafuta matakwa yake.

**Kuumia moyoni**

Hiki ni kizuizi kibaya sana kwenye mawasiliano. Kuna wakati mume au mke anaweza kukerwa na tabia au kauli za mwenzake. Wakati mwingine tabia au kauli hizi inaweza kuwa ndogo, lakini zikatafsiriwa vingine na mmoja kati ya wanandoa. Kwa baadhi ya wanandoa kauli au tabia hizi zinaweza kuwa sababu tosha ya kuvunja mawasiliano.

Ni vizuri wanandoa kuwa wakweli kwa nafsi zetu. Kama unahisi kuwa umemuudhi mwenzako kwa tabia au kauli zako, ni vema ukajitahidi kumuomba radhi. Lakini pia kama mwenzako amekuudhi ni vema kumwambia kwa upendo, staha na busara. Kwani mkosaji harekebishwi kwa matusi au vinginevyo. Kuna wakati unaudhiwa na mpenzi wako, wakati mpenzi wako hajui kwamba amekuudhi.

Hivyo, ukitegemea yeye akuombe radhi utaamini kuwa hakupendi, kwa sababu hatafanya hivyo kwa sababu hajui kama amekuudhi. Mtu anapoamua kuzira au kususa au kuuchuna (kwa Kiswahili cha leo) katika hali kama hii, anakuwa hajitendei wala kumtendea mwenzake haki.Ni muhimu unapoona umeudhiwa au kutoridhishwa na mienendo fulani ya mwenzako, mweleze mwenzako kwa upendo na staha badala ya kunyamaza na kufanya visa.

Chagua mahali na muda mwafaka wa kumweleza kwani si kila mahali na muda unaofaa kuzungumza mambo nyeti. Mweleze mwenzako unachofikiri juu yake. Unapofanya hivyo, zingatia kwanza hali (mood) ya mwenzako. Inashauriwa kwamba, wakati mtu akiwa katika hasira, majonzi au wasiwasi; amechoka au njaa siyo vizuri kuzungumza naye hisia zako au kero. Muda unaofaa ni ule ambao anakuwa amepumzika (relax).

Mahali panapofaa ni pale ambapo mnaweza kukaa wawili kwa faragha pasipo kusumbuliwa na yeyote. Isipokuwa unaweza kuzungumza na mwenzako wakati na mahali popote kama nia ni kumsaidia mwenzako kutoka katika hali hizo za hasira, majonzi au wasiwasi n.k, kwani inawezekana ikawa ni hali isiyohitaji kusubiri au itifaki fulani. Kufanya hivyo, ndiyo mawasiliano yenyewe na kushindwa kufanya hivyo maana yake ni kushindwa katika mawasiliano.

Ikumbukwe kuwa, matatizo au migogoro mingi katika ndoa au uhusiano wa watu, huweza kabisa kuletwa au kuchochewa na kukosekana kwa mawasiliano. Jifunze kuwasiliana na mwenzako. Bruce na Carol Britten katika Kitabu chao kiitwacho, "Answers for your Marriage" wanasisitiza wakisema:

*"Your marriage will become more romantic as you choose to communicate with each other, and love one another unselfishly."*

Jifunze kuzungumza na kusikiliza kwa upendo. Ni muhimu kuwa na juhudi katika kujenga mawasiliano. Ni dhahiri kuwa, kadri wanandoa wanavyowasiliana, ndio wanavyozidi kufahamiana na kuongeza thamani yao. Wanandoa wajifunze kuwa na mawasiliano bora zaidi kati yao kuliko kwa mtu mwingine yeyote ili kujenga ndoa imara.

**■ Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

SEPTEMBA 26, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Mkate wa nyama una ladha tamu



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Zijue mbinu za kupambana na mchwa baada ya ujenzi




## KATUNIKA

Ukurasa 16




# PUA YA UREMBO

## Namna ya kuondoa chunusi

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | S | W | A | L | A |
| ■ | U | ■ | ■ | E | ■ |
| O | K | A | ■ | G | ■ |
| ■ | U | ■ | G | E | A |
| ■ | M | ■ | ■ | V | ■ |
| L | A | U | M | U | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
JAA, DAU, SHIDA, BANGI, DAWATI, SHAMBA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO Ali alikwenda shambani na mama yake, walipofika walikata miwa na kuanza kula. Wakati wanakula Ali alikuwa akikusanya maganda ya miwa na kuyaweka ndani ya mfuko.

Mama: Ali kumbe umekua mwanangu, maganda unakwenda kuyatupa shimoni?

Ali: Hapana mama, nakwenda kuyaweka pale katika kichuguu

Mama: Kwenye kichuguu kuna nini?

Ali: Kuna wadudu Chungu pale, maganda haya watakula vizuri tu.

Mama: Ulijuaje kama wanakula maganda ya miwa?

Ali: Si mwalimu alitufundisha kuwa ganda la muwa la jana, chungu kaona kivuno.

Mama: Mwanangu huo ni msemo tu, una maana kuwa unachokiona wewe hakifai, wenzako wanakitamani.

SWALI

Mto Ruvuma unapita katika mpaka wa nchi gani kusini mwa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mifano ya watu waliotolewa kwenye nafasi au vyeo vyao

KARIBU tena msomaji kwenye gurudumu letu la Maisha Ndivyo Yalivyo. Tayari tumeshaona siri ya nafasi au cheo cha mtu kuchukuliwa. Nikasema kuwa nafasi yako ndio inayoamua hatma ya maisha yako.

Wiki iliyopita tuliangalia dalili za mtu aliyetolewa kwenye nafasi yake. Leo nitoe baadhi ya mifano ya watu waliotolewa kwenye nafasi zao pasipo kujua wakidhani ni jambo la kawaida kumbe yuko adui aliyejificha.

Yuko baba mmoja alikuwa mhudumu wa ofisi katika eneo la kufanya usafi. Kwa miaka mitatu hajawahi kwenda likizo. Kila akipewa likizo husema anaendelea kujitolea kwa kigezo kwamba anaipenda sana kazi yake. Akafikia hatua kusema mshahara wake wa likizo uwekwe kwenye akaunti yake.

Alikuwa akiaminika sana kwenye ofisi ile. Ikitokea mkurugenzi wa kampuni anataka kutoa uamuzi fulani inabidi wamwite huyo mhudumu wa ofisi na kumshirikisha na kile atakachoshauri kinapitishwa.

Mhudumu huyu akisema hili gari leo nataka nilitumie lisitoke, kweli inakuwa hivyo. Kumbe wakati haendi likizo kuna vitu huwa anafanya kwenye ile ofisi. Ameshikilia ile ofisi na kuchukua nafasi za watu wengine.

Ukienda kwenye biashara ndiyo usiseme. Utashangaa wewe una bidhaa nzuri, lakini mwenzako anauza kuliko wewe. Huyo tayari kashachukua nafasi yako ya kibiashara. Utaendelea kupiga miayo na kulalamika hakuna wateja, kumbe walishachukua nafasi yako siku nyingi.

Mfano mwingine ni mama mmoja kule Mwanza, mtaa wa Makoroboi alifungua duka. Akawa anauza vizuri lakini ghafla biashara ikaharibika. Badala ya yeye kuweka bidhaa, majirani zake wakawa ndio wanaleta bidhaa zao kuuzia hapo dukani kwake. Akaulizwa kisa cha kuruhusu hali hiyo kutokea hakuwa na jibu.

Yakafanyika maombi ya nguvu pale dukani. Siku moja mtu mmoja akawa anazunguka kwenye eneo la duka hilo kisha akaingia na kuuliza; hivi duka hili lilikuwepo? Akasema alishazunguka hapo mara nne akilishangaa lile duka kwani alikuwa halioni. Baada ya maombi giza likaondoka duka likaonekana.

Mama akaanza kupata wateja, tena kwa foleni. Leo amejenga nyumba yake kubwa. Nafasi yake ya kibiashara ilichukuliwa na watu wengine. Ukiona unafanya kazi kwa kutumia nguvu kubwa tambua ya kuwa nafasi yako imeshachukuliwa.

Watu wengi wapo kimwili sana, hawapo kiroho. Lazima uangalie hata ndoto unazoota. Kila siku unaota unafanya mitihani na wakati mwingine unafeli. Au unafanya mitihani kisha muda unaisha kabla hujamaliza maswali. Hapo ni dhahiri kwamba nafasi yako imeshachukuliwa na mtu mwingine.

Msomaji wangu, unapotoka kwenye nafasi, ule uwapo wa utukufu huondoka, hivyo kubakia mtu wa kawaida tu. Usifikiri ni kitu kidogo. Heshimu ile heshima uliyokuwa nayo. Jiulize ule utiisho uko wapi? Leo watoto wadogo wanakudharau kwa sababu huna chochote cha maana.

Mungu anapokupa nafasi na ukasimama imara, watu watakiri kweli huyu yupo kwenye nafasi yake. Ndiyo maana mtu akiwa kwenye nafasi yake anaheshimiwa. Uwezo wa Mungu huwa juu yake hata kama hawataki.

Huko ofisini ndiyo usiseme. Unapandishwa cheo kumbe hiyo nafasi mtu anaitaka. Anafanya kila ajuavyo na ghafla utendaji wako unashuka, bosi anakuchukia, wenzako hawakupi ushirikiano. Unachelewa kazini, hatimaye uongozi unakuondoa, kisa hutoshi.

Mama mmoja ndoa imekuwa na amani na kubahatika uzao watoto watatu. Kila mtu aliyewaona wanandoa hao aliwafurahia namna walivyokuwa wakipendana. Lakini ghafla ndoa ikatikisika, mume kapata mchepuko akahama kabisa nyumbani.

Mama akawa mtulivu na kuendelea na biashara ya duka la nguo pale Ngarenaro, Arusha. Tatizo linakuja yule mume anamtolea maneno ya ukali akimwambia ajiandae kuondoka kwani atakuja na dogo dogo hapo nyumbani. Hata hivyo, mama huyu ameapa haondoki hata iweje. Hapa nafasi yake imeshachukuliwa.

Watu wengi wanahitaji sana nguvu ya Mungu kusimama kwenye nafasi zao. Hakuna jambo linalotokea kwa bahati mbaya pasipo chanzo. Mama asiposimama kwenye nafasi yake, na zaidi sana kumuombea mumewe ni rahisi sana nyumba kubomoka. Maisha Ndivyo Yalivyo.

**Wiki ijayo tutaangalia jinsi ya kurudishwa kwenye nafasi yako. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe mfupi 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Bila kuimarisha sekta binafsi tatizo la ajira litaendelea kuitafuna Tanzania

MOJA ya manufaa ya safari ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhudhuria Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ni kukutana na viongozi wakuu wa mashirika makubwa ya kimataifa.

Viongozi wakuu aliokutana nao na kufanya mazungumzo ni pamoja na Rais wa Benki ya Dunia (WB), David Malpass, ambaye alionyesha nia ya kuisaidia Tanzania kuinua sekta binafsi kupitia tekonolojia.

Hii ni habari njema kwa Tanzania kwa kuwa hakuna ubishi kuwa sekta binafsi inajikongoja huku ikiwa ndiyo injini ya uchumi kwa kuwa inaweza kuajiri Watanzania wengi. Hiyo ni kutokana na ukweli kuwa mabadiliko ya kiuchumi hayajawezesha serikali kuajiri kila Mtanzania mwenye sifa ya kuajiriwa.

Mathalani, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2019/20 ilitoa tathmini ya tatizo hilo kuwa kupungua kwa uwekezaji kumekwaza ajira.

Alisema miradi mipya katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ilipungua kwa wastani wa nusu na ndiyo ulikuwa uhalisia wa mwenendo wa ajira nchini kwa miaka mitano iliyopita.

CAG alisema ndani ya kipindi hicho ajira zilipungua kutoka waajiriwa 63,223 mwaka 2015/16 hadi 32,115 mwaka 2019/20 sawa na asilimia 48.

Aidha, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Dar es Slaama, Prof. Honest Ngowi, Julai, mwaka huu, alinukuliwa akiishauri serikali ipitie sera, sheria na mikakati yake kwa kuwa zamani iliajiri wengi lakini kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, ajira nyingi zimehamia kwenye sekta binafsi.

Alisema ni muhimu serikali ikaweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kushiriki shughuli za uchumi na uwekezaji ili kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania hasa kwa kujiajiri.

Juni, mwaka huu, Rais Samia alizungumza na vijana jijini Mwanza na alieleza kuwapo kwa upungufu wa vijana waliopo kwenye ajira. Alisema vijana nchini wako milioni 20.7 ambao ni wenye umri wa miaka 15-35, lakini ndani ya kundi hilo, asilimia 11.4 wenye sifa za kuajiriwa hawako kazini.

Ripoti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ya Agosti 14, 2019 ilibainisha kiwango cha ajira kilipungua kwenye sekta binafsi kutoka waajiriwa 239,019 mwaka 2016/17 hadi ajira 137.054 mwaka 2017/18.

Kwa hali hiyo, taarifa za WB kuisaidia sekta binafsi ni habari njema kwa Watanzania kwa kuwa sasa tunashuhudia ukuaji wa tekonolojia na ongezeko la ajira. Kazi inabaki kwetu ni kwa kiasi gani tutapokea na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta hiyo kuchanua?

Bila kuwa na sekta binafsi imara hakuna maendeleo kwa kuwa idadi ya wasio na ajira itaongezeka maana yake wengi watakuwa hawawezi kumudu mahitaji ya msingi, hawachangii uchumi wa nchi, hawana uwezo wa kupata huduma za afya na elimu, jambo ambalo linaweza kuongeza matukio ya uhalifu.

Tatizo la ukosefu wa ajira linatofautiana nchi hadi nchi kwa kuwa zile zilizoendelea zimejitahidi kuweka sera na sheria nzuri za kukuza sekta binafsi ambayo imetoa ajira nyingi kwa watu wake kiasi kwamba watu huchagua aina ya kazi ya kufanya lakini si kwamba hakuna ajira kabisa.

Tatizo kubwa ni kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania ambayo kwa sasa ina kazi kubwa ya kuinua upya sekta binafsi ambayo ilipooza kiasi cha wengi kufunga kampuni na biashara na wengine kuondoka kabisa nchini kwa sababu mbalimbali.

Kutokana na vikwazo hivyo, Rais Samia Suluhu Hassan aliona umuhimu wa kuimarisha Wizara ya Uwekezaji ambayo imewekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu lengo likiwa ni kushughulikia matatizo yote.

Kwa sasa wizara hiyo inajisifia kuongezeka kwa wawekezaji nchini ikiwa na tafsiri ya kuongeza ukuaji wa uchumi na ajira kwa Watanzania, ingawa ni muhimu kufuatilia kwa kina ni aina gani ya ajira ambayo inahesabiwa kama ni yenye tija kwa mtu mmoja mmoja na taifa au la.

Lazima jitihada za makusudi zichukuliwa kuisaidia sekta binafsi ambayo ujenzi wake ulianza wakati wa serikali ya awamu wa nne na ilionekana kustawi kiasi cha mamilioni kupata ajira.

Bila kuwa na sekta binafsi imara maana yake uchumi utasimama au utayumba kwa kuwa serikali haiwezi kuajiri wote wenye sifa na ndiyo maana inajulikana kama injini ya uchumi wa nchi yoyote duniani na kama ikipuuzwa na kuumizwa wengi watakosa ajira na hata mchango wake kwenye uchumi hautaonekana.

Wanaomaliza vyuo vikuu katika ngazi mbalimbali wanaongezeka na kwa muundo wa elimu yetu, wengi hawajaandaliwa kujiajiri bali kuajiriwa. Huu ni ujumbe kwa serikali kwamba inapaswa kuona hili na kuja na mabadiliko makubwa ya mitaala yenye mawazo ya sekta binafsi juu ya namna bora ya wahitimu kuwa watengeneza ajira.

Iliwa tutakuwa na watengeneza ajira maana yake tutapunguza idadi ya wasio na ajira nchini, lakini tutaongeza wanaochangia uchumi wa nchi na kuondoa wategemezi, lakini hilo linawezekana ikiwa kutakuwa na nia thabiti ya watendaji serikalini kuinua sekta binafsi badala ya kuididimiza kupitia mamlaka walizo nazo.

**Mungu ibariki Tanzania**



Agosti 28, mwaka huu ilikuwa siku ya furaha kwa Mbonde Kiligito baada ya kufunga ndoa na Amne Chusu. Sherehe ya kuwapongeza ilifanyika katika ukumbi wa Lamada jijini Dar es salaam.

## MITINDO

Na Christina Mwakangale



# NGUO ZA HARIRI ZINAVUTIA

NGUO zilizotengenezwa kwa vitambaa vya hariri ni maarufu sana kwa wanawake wengi ambao wanapenda kuwa tofauti.

Hata hivyo, nguo hizo zinakuwa na mwonekano wa kipekee na kumfanya mvaaji kupendeza zaidi pale anapokutana na wengine.

Hufaa zaidi kuvaliwa katika nyakati na majira maalum kutokana na upekee wake.

**MAJIRA YA JOTO**

Wakati mzuri wa kujimwaga na nguo za aina hii ambazo zina mng'ao wa kupendeza ni wakati wa joto la wastani.

Vazi hili halitaki jua au mwanga mkali, inapendeza zaidi kuvaliwa wakati wa mwanga hafifu ili kuruhusu mng'ao wa hariri kuonekana kwa urahisi.

Hata rangi ya nguo isiwe ya kung'aa sana, kwa mfano unaweza kutumia nguo yenye rangi ya kijivu, maziwa, pinki au samawati.

**VAZI LA JIONI.**

Kwa kawaida vazi la hariri linalovaliwa jioni linakuwa refu na lenye nakshi nyingi zinazonogesha umbo la mwanamke.

Hapa unatakiwa kuwa makini na hali ya hewa kama ya baridi, vaa nguo nyenye rangi nzito ili kufanya mwili kupata joto na pia kukupa mwonekano mzuri.

Kama kipindi cha joto, vaa nguo laini na yenye mwanga kiasi kwani itakufanya kuwa na furaha





UREMBO

Na Mary Geofrey



# PUA YA UREMBO

## Namna ya kuondoa chunusi

PUA pamoja na kuwa kiungo muhimu katika kazi ya upumuaji kwa binadamu, lakini ina kazi nyingine kubwa ya kutafsiri urembo wa mtu.

Hata hivyo, kiungo hiki utunzaji wake upo tofauti na inahitaji umakini kwa ajili ya kuhakikisha inakuwa salama zaidi.

Tatizo la ngozi iliyokufa inayokutana na hewa ndani ya pua inasababisha kuota vipele ambavyo huwa kero.

Vipele hivyo aina ya chunusi huwatokea zaidi watu wenye ngozi za mafuta kwa wanawake na wanaume.

Unaweza kuziondoa chunusi hizo kwa njia za asili ambazo kila mmoja anaweza kufanya akiwa nyumbani kwake.

Unachotakiwa ni kuosha uso wako mara mbili kwa siku na maji ya uvuguvugu.

Baada ya kuosha fanya kama unapigapiga taulo usoni usisugue. Hii ni njia inayopunguza uchafu na mafuta kujijenga kwenye mashimo ya ngozi.

Mvuke ni njia nzuri ya kuondoa vipele, unachotakiwa kufanya ni kuchemsha maji kisha uyamimine kwenye bakuli.

Hii ni njia nzuri ya kufungua tundu au vinyweleo kwenye ngozi ambapo inakuwa rahisi kuondoa uchafu kwenye ngozi.

Ukitoka kuoga, tumia vidole vyako viwili kusugua taratibu eneo la pua, itaondoa ngozi zote zilizokauka.

Epuka kujishika eneo hilo wakati wote kwa sababu vijidudu vilivyopo kwenye mikono vinasababisha hali hiyo kuendelea au kuongezeka.

**ALOE VERA**

Changanya matone matatu ya juisi ya limau na jeli ya Aloe vera. Weka kwenye uso, kisha sugua taratibu kwa robo saa. Baadaye safisha uso kwa kutumia maji moto.

**NYANYA**

Tengeneza juisi ya nyanya, chukua na upake usoni mpaka ikauke. Kisha osha uso kwa maji ya uvuguvugu.

**SUKARI**

Saga sukari kisha changanya na juisi ya limau, weka kwenye eneo la pua na usugue taratibu. Baada ya dakika 20 osha hapo pua yako itakuwa safi.

**MAYAI**

Mayai yana omega-3 fatty acids nyingi, vitamini na madini ambayo husaidia ngozi. Chukua kiini cha yai weka kwenye uso, ukishakauka osha uso wako na maji ya uvuguvugu.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mkate wa nyama una ladha tamu

MKATE wa nyama ni chakula kizuri, kitamu na rahisi kuandaa.

Chakula hiki unaweza kula na aina yoyote ya kinywaji au kula muda wowote iwe asubuhi, mchana au usiku .

**MAHITAJI**

Butter vijiko vitatu, vitunguu maji vitatu, figili fungu moja, Karoti mbili, vitunguu saumu viwili, chumvi vijiko viwili vya chai, pilipili manga kijiko kimoja cha chai, nyama ya kusaga kilo mbili inaweza ikawa ya ng'ombe, kondoo au yoyote.

Mahitaji mengine ni majani ya kotimiri (parsley), mayai mawili, worcestershire sause vijiko viwili, hiliki, vitunguu maji, maziwa robo lita na tomato.

**NAMNA YA KUANDAA**

Bandika sufuria weka mafuta mgando (butter) acha iyeyuke. Kisha weka vitunguu maji, carrot na figili, pika mpaka vilainike kisha punguza moto, weka vitunguu saumu na katia na vitunguu vya majani, pika kwa sekunde 30.

Ongeza hiliki na nyanya ya kopo, koroga mpaka uhakikishe vimeiva kisha epua.

Chukua bakuli kubwa, weka nyama, mayai, chumvi, pilipili manga, mkate, maziwa na zile mboga ulizopika.

Changanya vizuri ila tumia mikono kuchanganya mpaka vichanganyike vizuri, na uhakikishe viungo vimeshika vizuri kwenye huo mchanganyiko.

Weka mchanganyiko kwenye chombo utakachotumia kuokea, ni vizuri ukatumia chombo cha kuokea mkate.

Mwagia 'ketchup' kwa juu ya mchanganyiko, sambaza kwa juu mpaka ienee vizuri kisha oka.

Oka kwa dakika 45 kisha utoe, mwagia tena tomato kwa juu na uisambaze. Rudisha tena kwenye oven kwa dakika 15, epua iache ipoe.

Baada ya kuiva utenge kwa dakika 10 na hapo utakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Zijue mbinu za kupambana na mchwa baada ya ujenzi

LEO tunajifunza namna ya kupambana na mchwa baada ya ujenzi wa nyumba.

Mdudu huyu amekuwa tishio kubwa katika ustawi wa nyumba na husababisha uharibifu mkubwa asipodhibitiwa.

Ziko mbinu mbalimbali za kupambana na mchwa baada ya kujenga nyumba ambazo zinatajwa na mtaalam katika sekta hii kutoka Bunju B Dar es Salaam, Peter Kweka.

Kweka anasema namna ya kudhibiti mchwa kwenye nyumba baada ya ujenzi kabla ya kuanza kuitumia ni lazima yote inyunyiziwe dawa ili kuua mazalia yote ya mdudu huyo.

Anasema kudhibiti mdudu huyo wakati tayari unaitumia nyumba kunaweza kuleta usumbufu kidogo tofauti na ilivyo kwa nyumba ambayo haijaanza kutumika.

Mtaalamu huyo anashauri kwamba ni vyema mtumiaji au mmiliki wa nyumba kuweka utaratibu na mazoea ya kuweka dawa kila baada ya muda fulani kupita.

"Kabla ya kutumia dawa hizi za kuilinda nyumba yako dhidi ya mchwa ni vyema ukapata ushauri wa mtaalamu wa ujenzi au kilimo na mifugo. Kuna aina nyingi za dawa zinazotumika kwa sasa na bado zingine zinaendelea kubuniwa kuendana na ukuaji wa sayansi na teknolojia ya utengenezaji wa dawa.

"Ni vyema kutumia dawa kwa kuzingatia maelekezo ya mtaalamu au mzalishaji wa dawa hizo kwa sababu hazifanani katika mbinu za matumizi, hivyo usiige tu kutoka kwa wengine. Ni vyema kupata kwanza ushauri," anasema.

Pia anaelekeza kwamba kabla ya kuweka dawa kwenye nyumba, unapaswa kusafisha mifereji na kuhakikisha hakuna mabomba yanayovuja ikiwamo kukausha maeneo yote yenye unyevunyevu.

Sambamba na hilo, anashauri kuweka dawa kwenye maeneo yote ambayo ni njia au makazi ya mchwa na ambayo ni chanzo hata kama hakuna mchwa wanaoonekana.

Njia nyingine ni kung'oa na kuondoa mbao zote zilizoharibiwa na mchwa na kuweka nyingine pamoja na kutoruhusu mbao zozote zigusane na udongo wowote au unyevunyevu kwa muda mrefu na kuziba matundu yote kwenye sakafu na kuta.



## Namna ya kuchagua vitambaa vya mezani



MEZA ya chakula haijakamilika kama itakuwa haina kitambaa juu yake. Kitambaa cha mezani ni moja ya alama ya umaridadi na usafi hivyo ni muhimu kufanya chaguo zuri. Zifuatazo ni dondoo za namna ya kuchagua vitambaa bora vya meza ya chakula.


1: Kitambaa cha pamba ni kizuri kuweka mezani kutokana na ukweli kwamba kilianza kutumiwa kwa miaka mingi. Aina hiyo ya kitambaa ina mwonekano wa kuvutia, na kinahifadhi unyevunyevu pale chakula kinapomwagika, pia kinafuliwa kwa urahisi zaidi kwa kutumia sabuni ya kawaida.

2: Kitambaa cha mafuta. Ni kitambaa chenye mchanganyiko wa plastiki kiasi, hiki kinafaa kuweka mezani kutokana na faida yake ya kusafishwa kwa urahisi kwa kufutwa pale inapomwagikiwa na chakula.

3: Kitambaa cha Silicone ni kizuri kwa mwonekano na kuipamba meza, lakini unatakiwa kuwa makini kuchagua rangi na ukubwa wake kwani huwa hakikai vizuri kutokana na malighafi yake.

4: Kitambaa cha leso ni aina ya mapambo ya kale zaidi, kwani kitambaa huwekwa katikati ya meza kwa sababu zina ukubwa mdogo.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
WANANCHI WANGU HAWANITAKI NIENDE MARA KWA MARA JIMBONI KWANGU... KWA SABABU...
SIWAMWAGII CHANGA-RAWE BARABARANI BALI NAWAMWAGIA FEDHA MAJUMBANI WANAOGOPA KUKABWA!
MKAVUUUU! HATA UCHEKI ULIVYOZOEA 'FIKSI'
MWANASIASA HUNA TIMU LAKINI MBONA KAMA PRESHA?
UNAJUA UKINITIBUA NITAKUBAMIZA NSHAVURUGWA SIELEWI!!
KILA MECHI YA WATANI IKIFIKA NAJIKUTA LINA-DAI KUTUMIKA!
USHABIKI NA HILI, NI SAWA NA PETROLI NA KIBERITI
POLISI
NDANI YA KIBASI
JAMANI YALIISHIA KWA NKAPA!
NANI AFUNDWE KAMA MNABISHA MECHI IRUDIWE MUONE! EBO!
MPERA'MPERA MPAKA MKAJI-KUTA MNAONA GIZA TOTORO!
MMEZIDI KUTAMBA MMESHA-FUNDWA
KELELENIIII!
DEREVA PAKI PEMBENI TUZICHAPE!
ETI?
KILA MECHI YA WATANI IKIMALIZIKA LAZIMA UHAMISHE VITU, KWA NINI?
KWA SABABU 'TUNAPINGA'
SABUFA FENI SAHANI VIJIKO
ONESA MIMI ILE 'SIMBA' WATU INA-SEMA JANA ITAUA! ONESA MIMI...
YERO MBONA UNATAKA KUNIPA 'JAKAMOYO?' MIE MGENI HAPA
NIULIZE NJIA NIKUPELEKE HADI MLANGONI
'KAMBINI'
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...CHONGA FENICHA SIO MDOMO

HABARI KIMATAIFA

# Wagombea Ujerumani wamaliza kampeni

**BERLIN, Ujerumani**

KINYANG'ANYIRO cha kumrithi Kansela Angela Merkel, kinazidi kupamba moto nchini Ujerumani, baada ya wagombea wawili kuchuana vikali katika kura za maoni.

Utafiti wa maoni ya raia unaonesha kuna tofauti ndogo kati ya wagombea hao, huku Scholz wa chama kinachofuata nadharia ya mrengo wa wastani wa kushoto SPD akiongoza kwa kura tatu dhidi ya Armin Laschet, kutoka chama cha CDU.

Kansela anayemaliza muda wake, Angela Merkel, ambaye ameliongoza taifa lenye nguvu zaidi kiuchumi barani Ulaya kwa karibu miaka 16, anamuunga mkono mwanachama mwenzake wa chama cha CDU, Laschet, ambaye anamalizia mkutano wake kampeni katika eneo alilozaliwa la Aachen.

Scholz wa chama cha SPD, yuko kwenye kampeni za mwisho katika jimbo la Brandenburg, lililo karibu na mji mkuu.

Mgombea wa tatu kutoka chama cha kijani, Annalena Baerbock, amehitimisha kampeni zake akiwa kwenye nafasi ya tatu katika utafiti huo wa maoni, huku akipewa nafasi ndogo ya kuwa kansela.

Hata hivyo, chama chake kinatarajiwa kuimarisha zaidi nafasi yake kwenye uchaguzi huu ikilinganishwa na ule wa mwaka 2017, na huenda kikahusika katika kuunda serikali ya pamoja.

Waangalizi wengi wa uchaguzi wanatarajia matokeo yatasababisha kuwa na serikali inayohusisha vyama vitatu, lakini bado haijawa wazi ni vyama vipi vitakavyokuwemo. Ikiwa kambi ya Laschet, inayoundwa na vyama ndugu CDU/CSU kitaongoza, serikali ya muungano inatarajiwa kuwa ya mrengo wa kati na kulia.

Kama chama cha SPD kikishinda, basi Ujerumani inaweza ikabadilika kidogo au kuchukua mwelekeo mpya wa siasa za mrengo wa kushoto kutegemeana na ni nani atakayechaguliwa na Scholz kuwa mshirika wake.

Uwezekano mwingine ni kuwa Ujerumani inaweza kuendelea na serikali ya muungano wake wa sasa unaoundwa na vyama vya SPD na CDU/CSU

**DW**




Mfanyakazi wa zima moto akiwa katika jitihada ya kupambana na moto unaoendelea kuwaka na kuteketeza msitu uliopo karibu na Johnsondale, katika jimbo la California nchini Marekani, jana. **(PICHA: AFP)**

# Abbas aipa Israel mwaka mmoja kuondoka maeneo ya Palestina

**NEWYORK, Marekani**

KONGOZI wa Palestina, Mahmud Abbas, ameipa mwaka mmoja Israel kuondoka katika maeneo iliyoyakalia kwa nguvu la sivyo hatoitambua serikali ya Kiyahudi kulingana na mipaka ya kabla ya mwaka 1967.

Katika hotuba yake kwa njia ya mtandaoni kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Abbas alimtaka Katibu Mkuu Antonio Guterres, kuitisha mkutano wa kimataifa wa amani.

Hata hivyo, katika ombi hilo pia aliishurutisha Israel itajwe kuwa ni taifa lililochukua mamlaka kwa nguvu na kwamba ina mwaka mmoja wa kuondoka kwenye maeneo ya Wapalestina.

Maeneo hayo waliyochukuliwa kimabavu ni pamoja na Jerusalem Mashariki.

Mchakato wa amani wa kufikia suluhu ya kuwa na nchi mbili umekwama kwa miaka miaka mingi.

Israeli ilitupilia mbali dai la kiongozi huyo wa Palestina.

**DW**

# Ofisa afungwa jela miaka 40 kwa ufisadi

**KAMPALA, Uganda**

MAHAKAMA ya kupambana na ufisadi nchini Uganda, imemhukumu ofisa mmoja wa serikali kifungo cha miaka 40 jela na fidia ya dola milioni 5.4, baada ya kupatikana na hatia ya kupora pesa za kugharamikia mpango wa kusaidia kulijenga tena eneo la kaskazini mwa nchi hiyo liloathiriwa na migogoro.

Godfrey Kazinda alishtakiwa kwa ubadhirifu wa dola milioni 26.4 za mpango huo uliofadhiliwa na serikali za Ireland, Sweden na Denmark kusaidia kulifufua eneo hilo la Uganda lililoharibiwa kutokana na vita ya muda mrefu iliyosababishwa na waasi wa Lord's Resistance Army.

Serikali pia imekamata mali za Kazinda, ikiwa ni pamoja na jumba la vyumba 20 lenye thamani ya dola milioni moja, pamoja na magari manne ya kifahari yenye thamani ya dola 218,000.

Aidha polisi pia iligundua dola 273,700 zilizofishwa kwenye moja ya nyumba zake Kampala.

Hukumu hiyo ilitolewa baada ya kesi hiyo kuunguruma mahakamani kwa miaka tisa.

**DW.**

## Iran yaikosoa Marekani kutoa kauli mbili zinazokinzana

**TEHRAN, Marekani**

WAZIRI mpya wa Mambo ya Nje wa Iran, Hossain Amir Abdollah, amesema nchi yake iko tayari kurudi kwenye meza ya mazungumzo yanayohusu silaha za nyuklia. Hata hivyo, aliishutumu nchi hiyo kutoa kauli zinazokinzana, ikisema iko tayari kurudi kwenye makubaliano hayo ya mwaka 2015, lakini wakati huo huo ikiendelea kuiwekea Iran vikwazo vipya.

Katika mkutano na waandishi habari, Abdollah, alisema anatilia shaka nia ya kweli ya serikali ya Joe Biden, na kwamba kinachohitajika ni vitendo na sio maneno matupu ya kuvutia.

Abdollah alikosoa vikali vikwazo vya ziada ilivyowekewa nchi yake na utawala wa Biden, na pia kukataa kwake kuiruhusu Iran kuchukua pesa zake zilizohifadhiwa Korea Kusini na benki za Japan kwa ajili ya kununua chanjo za COVID-19 pamoja na dawa za binadamu.

**DW**

## Sudan yakamata mali za Hamas

**KHARTOUM, Sudan**

BAADA ya kuzimwa kwa mapinduzi nchini Sudan, serikali imetangaza kuvunja ushirikiano na kundi la Hamas la Palestina na kukamata mali zake zilizopo nchini humo.

Kikosi maalum kilichoundwa baada ya kuondolewa kwa kiongozi wa zamani wa nchi hiyo Omar al-Bashir, kilitangaza Alhamisi kwamba mali za kampuni kadhaa za kundi la Hamas linaloshikilia madaraka katika Ukanda wa Gaza zitakuwa chini ya serikali.

Mali hizo ni pamja na majengo, hoteli, hisa katika kampuni, kituo cha televisheni na ardhi ya kilimo.

Omar al-Bashir, aliunga mkono waziwazi kundi la Hamas dhidi ya Israeli na alikuwa ameiruhusu nchi yake kuwa ngome kuu ya kundi hilo, ambapo wanamgambo wa Hamas walipata hifadhi, kupata pesa au hata kusafirisha silaha.

Kukamatwa kwa mali hizo kunaashiria mabadiliko ya uongozi, na inaifurahisha marekani ambayo ilitoa sharti hilo ili kuiondoa Sudan katika orodha yake ya nchi zinazounga mkono ugaidi.

**RFA**

## MAKALA

# JINSI YA KUKABILIANA NA UKOSOAJI



Na Magabilo Masambu

NJIA bora kabisa ya kupunguza au kumaliza kile kinachoitwa ukosoaji bila madhara yoyote ni kupuuza mengi yasiyo ya kweli. Hii pia ni kwa sababu ukosoaji ni dhana inayotengenezwa na anayedhani kwamba anakosolewa, wakati upande wa pili kwa anayechukuliwa kama mkosoaji yeye huona kama anachokisema ni ushauri ili jambo fulani likae kama anavyotaka liwe.

Kwa hiyo tafsiri ya kile kinachosemwa kinaweza kuitwa ama ukosoaji au ushauri kutegemeana na anayekipokea. Anayeambiwa siku zote ndiye mwenye uchaguzi wa kukipa jina ama achukulie kama ukosoaji au ushauri kwake ambao pia anaweza kuufanyia kazi au kuuacha kutokana na mazingira ya jambo analosemwa nalo.

Zamani nilipokuwa mdogo nilikuwa nashangaa sana. Bahati nzuri nilishi na babu yangu nyakati za udogo wangu. Kuna jambo nilikuwa silielewi lakini sasa nimekuwa mtu mzima nina familia ndiyo nimeelewa. Lilikuwa jambo la kawaida babu yangu kutoshinda sana nyumbani, nikawa najiuliza mbona hii tabia ina wazee wengi? Hawapendi sana kushinda nyumbani na familia.

Leo nimekuwa na familia nikagundua kwamba kumbe ukipenda sana kushinda nyumbani mara nyingi utagundua vitu vingi ambavyo wakati haupo huwa vinachukuliwa kama vya kawaida. Lakini ukiwepo unaona kama ni upungufu, hivyo nafahamu sasa kwa nini wale wazee walikuwa hawapendi sana kushinda nyumbani na hii ni tabia ya wanaume wengi mara nyingi wanakwepa kuona udhaifu mwingi nyumbani badala yake wanaamua kushinda vijiweni kuepusha mengi.

Lakini kwa sababu naipenda familia yangu, nikasema siwezi kuwa nashinda vijiweni kwa kuwa kukaa na familia mbali hasa watoto naweza kujikuta napoteza upendo kwao. Madhara yake huwa hayaonekani ukiwa bado na nguvu za kufanya kazi bali ukizeeka na ukahitaji malezi ya watoto utakuta hakuna mwenye mpango na wewe kwa sababu hukutengeneza mapenzi kwao wakiwa wadogo.

Jambo kubwa ninalofanya ni kupuuza mambo mengi ninayoyaona yakitokea wakati nikiwepo. Najifanya kuziba macho na masikio huku nikiona na kusikia. Njia hii mara nyingi inampa taabu sana aliyetenda jambo ambalo angetegemea kuambiwa kwa nini unafanya hivi halafu haambiwi. Kwa vyovyote anaweza kupata hofu ya kutolitenda tena.

Nakumbuka nilipoanza shughuli za uandishi wa vitabu na makala mbalimbali miaka saba iliyopita, nilipata ushauri mwingi sana ambao kwa asiye na roho ngumu angechukulia kama ukosoaji. Ni kweli wakati mwingine inaumiza maana baadhi ya ushauri ulikuwa unanikatisha tamaa.

Kilichonisaidia ni kukubali kwamba sikuwa najua na kwa kuwa lugha ya Kiswahili pia niliifahamu nikiwa na umri wa miaka 16, nikagundua kwamba ndiyo maana inakoselewa sana. Kwa hiyo niliikubali hali hiyo na leo hii wale waliokuwa wakinikosoa ndio wanaonipongeza na ninawashukuru sana. Pengine wasingefanya hivyo, leo nisingekuwa mwandishi mzuri kama wanavyosema leo.

Nilichojifunza katika maisha tunahangaika sana na mabaya kuliko mema. Wako watu wanaoshauri mambo mema sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Kwanza hawajulikani na hakuna siku wamepata hata simu kutoka kwa viongozi serikalini ya kupongezwa kwamba mnafanya kazi nzuri, lakini siku wakiamua kutukana ndiyo siku watakayojulikana kwamba kumbe wapo.

Kwa hali ya dunia ilivyo, ni vigumu sana kudhibiti kinachoitwa ukosoaji na wakati mwingine nafikiri mila na desturi zetu za kiafrika zimetuathiri sana kuona kila jambo ni siri. Zamani ilikuwa ngumu sana kufahamu kama baba naye huwa anakwenda chooni! Alikuwa anaamka asubuhi mapema kabla hamjaamka, anawenda kujisaidia au mama kupata ujauzito ilikuwa siri kwa sababu alikuwa anaogopa kuulizwa na watoto mbona ana tumbo kubwa.

Lakini ugumu wake mwingine ni njia za upatikanaji na usambazaji wa habari zilivyorahisishwa. Tumejikuta mambo ya siri yanabaki machache tofauti na tulivyozoea. Kwa hiyo ni kukubaliana na hali kwamba hatuwezi kuwa kisiwa tukajitenga na dunia, japo tuna kila sababu ya kulinda utamaduni wetu bila kutumia nguvu nyingi. Nguvu hazijawahi kuzaa matunda ya muda mrefu.

Tusimlazimishe mbwa kwenda kula chakula kwa kumfunga kamba shingoni badala yake tufunge kengele na tuigonge siku ya kwanza anapokuja anakuta chakula, hivyo kila wakati akiisikia ile kengele anajua ni msosi huo hata siku ikigongwa kwa bahati mbaya hakuna chakula atoke mate ya kutamani kula chakula ndivyo alivyokuwa akifanya Ivan Pavlov.

Jambo fulani likizungumzwa likapuuzwa huwa mzungumzaji haendelei tena lakini yale tunayoona kwamba ni kweli hatufanyi vyema na yanahitaji mabadiliko kwa maslahi ya nchi ni kuyafanyia kazi bila kujali kwamba anayeyasema ni nani kwa sababu katikati ya mashetani hawawezi kukosekana malaika. Pamoja na ubaya wa watu wa Sodoma na Gomora, walipatikana watu wanne wema na wangelipatikana watano tu mji mzima usingechomwa moto kwa ajili yao.

Mara zote tukipenda kusikia mazuri tu kutoka kwa marafiki zetu wa karibu, hatutapata kujua udhaifu wetu. Badala yake tutapata habari za kufurahisha pekee ili tuwape vyeo wanaotufurahisha na ni vigumu sana kuendelea kimawazo kwa sababu tunakua tumejifungia.

Waliokuwa wakinikosoa kwenye uandishi wangu baadhi walikosoa na kunishauri namna bora ya kufanya. Wengine waliishia kukosoa tu na sikuwahi kuwalaumu kwa sababu tayari wanakuwa wameshaonyesha eneo linalohitaji marekebisho. Si lazima washauri namna ya kufanya, hiyo ilibaki kwangu ama kufanyia kazi au kuacha kama ilivyo na sikuwa napuuza yote.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Vituko vya Kiboko Msheli, timu za mitaani*



Na Adam Fungamwango

KWA sasa timu za mitaani hazina nguvu sana kama zile za miaka ya 1980 hadi mwishoni mwa miaka ya 1990.

Ni miaka ambayo soka la Tanzania lilikuwa juu sana, ambalo lilianzia miaka ya 1960, kiasi cha nchi hii kuwa juu sana kimichezo.

Leo tutaziangalia klabu na timu zao za mitaani. Zilikuwa na nguvu sana kama vile unavyoona Simba na Yanga sasa hivi. Wakazi wa maeneo yanayozunguka hizo timu wanafanya kila njia kuzisaidia ili kufanya vizuri na zilikuwa na mashabiki wengi waliokuwa wakiambatana nazo kwenda uwanjani. Wako waliokuwa mashabiki wa kawaida na wengine hawakuwa na kawaida.

Moja ya timu maarufu sana Dar es Salaam miaka ya 1980 hadi katikati ya miaka ya 1990 ni Kiboko Msheli. Klabu hii ya mpira makao makuu yake yalikuwa Magomeni Makuti. Haikuwa maarufu si kwa ajili ya mpira tu uwanjani bali pia ilikuwa na mashabiki wakorofi na wababe. Walikuwa na uwezo wa kufanya kitu chochote na wakati wowote ule sehemu yoyote ile.

Kwa wakazi waliokuwa wanaishi maeneo ya kuzunguka Magomeni kama Tandale, Manzese, Mwananyamala, Sinza, Kigogo na Mburahati, hata kama si mashabiki wa soka, walilazimika kujua ratiba ya mechi za mchangani ambazo Kiboko Msheli itacheza. Si kwa sababu walikuwa mashabiki bali kujihami kiusalama na mali zao.

Ilifika saa 8:00 mchana, basi wafanyabiashara watafunga maduka na sehemu zote za biashara zitafungwa kuwapisha mashabiki wa timu hiyo ambao walikuwa wakitoka kwa maandamano kutoka klabuni kwenda kucheza mechi zao za vikombe mitaani na kurudi.

Ndiyo timu pekee ambayo mashabiki wake wanakimbia mchakamchaka wakati wa kwenda kuangalia mechi na kurudi pia. Walifanya hivyo iwe timu imeshinda au kufungwa. Kilichotakiwa tu hapo ni kwamba maeneo yote wanayopita maduka, au biashara zote ziwe zimefungwa, vinginevyo ni halali yao. Ubabe wa mashabiki hao haukuwa mitaani tu bali hata uwanjani. Si mara zote mechi zao zinamalizika kwa dakika 90. Mashabiki wao wako tayari kufanya chochote wanapoona mwamuzi anawaonea.

Hiyo ikasababisha timu hiyo kukataliwa kuingizwa kwenye michuano mbalimbali iliyokuwa inaandaliwa. Nao wakawa wajanja sana. Wakikataliwa hubadilisha jina. Mpaka waandaaji kuja kujua kuwa timu ile ni Kiboko Msheli, tayari imeshacheza mechi moja au mbili.

Walipenda sana kutumia jina la Jamaica FC, pale wanapoona huenda wakakataliwa waliandikisha jina lao asili kutokana na fujo zao. Pamoja na yote walikuwa wanakubaliwa kutokana na mbwembwe na hamasa zao kwenye soka hasa uswahilini.

Kiboko Msheli ilitoa wachezaji wengi kucheza Ligi Kuu, na hasa wengi wao walikuwa anakwenda kuchezea klabu ya Sigara, mmoja wao akiwa ni straika hatari, aliyecheza na kuvuma kwa muda mfupi tu, Kessy Ramadhani 'Patel'.

Timu zingine zilizovuma ni Boom FC na Ashanti zote za Ilala. Ashanti ni timu maarufu kuliko Boom kwa sasa kwa sababu imeshacheza Ligi Kuu. Timu hizi upinzani wao ni kama Simba na Yanga miaka hiyo. Mechi ikichezwa Uwanja wa Karume kunakuwa na ulinzi mkali sawa na 'dabi' ya Kariakoo.

Timu zingine zilizovuma sana miaka hiyo ni Cargo, Abajalo ya Sinza, Sifa Politan ya Mtoni, Six Batallion, Black September ya Tandika, Faru Dume ya Manzese, Gerezani Star ya Kariakoo na Bongoyo FC ya Msasani.

Zingine ni Sea Breeze, Future ya Manzese, National ya Tandale, Chafosi Chaigoda ya Bagamoyo, Wacheche ya Ilala, Nevada ya Tandale, Kagera Rangers ya Manzese, Magomeni Kondoa FC, Les Leopard, Nzige Army, Sakramento ya Temeke, halafu kuna Batafongo ya Temeke Kota.

Pia kulikuwa na timu za Shavee, Briston City, Vive Style, Polisario, Black Six, Palestine, Uruguay, Great Olympic, Super Mzamba, Seven Blue Star, Opec, Berlin ya Tandika, Kitintale ya Bombom Kijiwe Samli, Santiago Chile ya Buguruni, African Temeke na Good Hope zote za Temeke, Avengers ya Mwenge, Keko Staff.

Kulikuwa na timu za Black People ya Majumba Sita Ukonga, TP Ibo au maarufu kwa jina la 'Kumkomanyani Giladi', TP Vita ya Kipawa, Msikate Tamaa na Mogo FC.

Kawe kulikuwa na timu za Ukwamani FC na Kawe Rangers, Mwananyamala kulikuwa na Flamingo FC na Bonde FC. Pia kulikuwa na timu za Santos, Pool England, Shangwe ya Ilala, Everton, Ajax, Maputo, Osibisa, Bungoni Fresh, Shekilango DC, New Kenda ambayo ni timu ya Jeshi la Wananchi, Sifa United iliyowatoa Madaraka Selemani na mdogo wake Idd Selemani hadi kuja kuichezea klabu ya Simba.

Care Boys ilikuwa timu ya eneo ya Kinondoni Biafra, lakini kulikuwa na timu za Eleven Killers na Ugimbi United zote za Kurasini, Ngurumo na Ukombozi zote za Kigogo Luhanga, Machava FC, Nondo, TP Nyundo, Shoka Afrika zote za Mwananyamala, Batafogo ya Tandaka na Asanta Tololo na Al Aswan zote za Kariakoo.

Mikoani nako hakukuwa nyuma, kulikuwa na Jamaica ya Morogoro, Mau Mau ya Chumbageni Tanga, Sungura FC ya Kyela Mbeya, Ombwezi ya Singida, Waya Mkali, Home Boys, Esso Arusha na Ololo Rangers zote za Arusha.

Pia kulikuwa na timu za Kiloleni Rangers, Ibadan na Torabora, zote za Tanga.

Hizi ni chache tu, kulikuwa na timu nyingi ambazo hazikuorodheshwa na mashabiki walikuwa wakijaa viwanjani kwenda kuzishangilia timu zao. Mbali na baadhi ya matatizo na changamoto za hapa na pale, lakini kulikuwa na burudani kubwa kwa kuangalia timu hizo, vituko na mbwembwe za mashabiki wao.

**Kwa maoni piga 0716 350534**

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-25

**Na Adam Fungamwangwo**
**(0716 350534)**

Nadhani tufanye kitu kimoja tu, tuwapigie Mamlaka ya Mawasiliano watupe umri sahihi wa Peterson Donald kitu ambacho tulisahau." Koplo Andrew alishauri.

Alipokubaliwa aliondoka. Dakika moja baadaye alirejea kikaoni. "Miaka yake ni 65." Aliwaambia wenzake.

"Sasa ni hivi. Kama baba yake mzazi Donald yuko hai, nadhani tuanze naye. Tumfuatilie. Nadhani kama yupo, ni kuichukua tu simu yake, inaweza kutupa kila kitu." Yalikuwa ni maneno ya Inspekta Andrew."

"Ina maana baba anaweza kumuua mkwewe kweli?" Afande mmoja akahoji.

"Nishawahi kusikia hadithi moja ya kijana anataka kumuoa msichana fulani, lakini msichana huyo akauawa na baba wa kijana huyo kwa sababu ya wivu wa kimapenzi. Kumbe alikuwa ni mchepuko wake. Dunia ina mambo hii. Usiione hivi." Aliongeza mmoja wa maafisa hao wa polisi na wakamaliza kikao chao.

*******************************

"Hallo, inspekta Andrew hapa naongea." Yalikuwa ni maneno ya mwanzo mara baada ya kupokea simu yake ya mkononi.

"Donald unasemaje?" Akauliza.

"Afande mimi nimeshapewa ruhusa hapa. Lakini hawa maafande wanaonilinda hapa wamesema hawawezi kuniruhusu mpaka wewe uamuru." Ilikuwa ni sauti ya Donald ambaye alikuwa bado kwenye Hospitali ya Mwananyamala, akiguza majeraha ya ajali aliyoipata.

"Kwani unataka kwenda wapi?"

"Nyumbani inspekta, unataka nikae hapa milele?"

"Hapana, nilikuwa nasema hivyo kutokana na usalama wako. Kumbuka kuwa hao askari wamekaa hapo kwa ajili ya kukulinda. Ni wewe mwenyewe ulisema kuna watu wanakufuatilia."

"Ndiyo ni kweli, lakini nilikuwa nahitaji kuondoka hapa ili nikafanye mipango mingine. Kumbuka afande hata mimi nalazimika kutafuta ushahidi mwingine. Huo mlionao ni mimi ndiye niliyewapa. Na hapa kuna kitu nafuatilia, inawezekana kabisa nikapata mwingine na kukurahisishieni kazi."

Mwanzo Inspekta Andrew alikuwa na wasiwasi. Hii inatokana na baadhi ya wenzake kumtilia shaka Donald kuwa huenda ndiye akawa muuaji. Ni yeye ndiye aliyekuwa anamtetea. Mashaka yake ni kwamba Donald anaweza kutoroka, au kuuawa. Chochote kitakachotokea kati ya hicho lawama inaweza kuwa kwake.




**"Ndiyo ni kweli, lakini nilikuwa nahitaji kuondoka hapa ili nikafanye mipango mingine. Kumbuka afande hata mimi nalazimika kutafuta ushahidi mwingine. Huo mlionao ni mimi ndiye niliyewapa. Na hapa kuna kitu nafuatilia, inawezekana kabisa nikapata mwingine na kukurahisishieni kazi."**

Baada ya mazungumzo yapatayo dakika 15 hivi, Inspekta Andrew alimwambia Donald ampe simu mmoja wa askari kanzu waliokuwa wodini.

"Kama amesharuhusiwa, basi na nyinyi ondokeni, mwacheni aende zake. Lile tishio la usalama wake sasa halipo." Aliamuru.

Alitoka nje ya Hospitali ya Mwananyamala. Ilikuwa ni saa 12:00 jioni, wakati tayari wale wote ambao walikuja kuwaona wagonjwa, wameshaambiwa waondoke.

Ni muda ambao kwake aliona ni mzuri kwa sababu, tayari baadhi ya ndugu zake wameshakuja kumtazama pamoja na wazazi wake, wakaondoka. Hakuna aliyejua kuwa siku ile nzima tayari alikuwa amesharuhusiwa.

Hii ilimpa fursa ya kukodi bodaboda ambayo ilimchukua hadi nyumbani kwao Mbezi Beach. Alisalimiana na ndugu zake ambao walishangaa kumuona amerudi ghafla, kwani walimuacha amelala hospitalini.

Baba yake mzee Peterson hakuwepo. Mama yake alikuwepo. Alionekana kuwa na huzuni. "Mama usiwe na wasiwasi, mimi nimekusamehe kwa yote. Haya mliyoyataka ndiyo yanayosabisha na mimi kutaka niuawe. Haikuwa ajali ya kawaida. Ilikuwa ni ya kutengeneza. Lakini kwa sasa ni mapema sana. Kuna kazi nataka niifanye, ila nakuhakikishia mama yangu utakuwa salama." Alisema akimkumbatia mama yake.

"Nisamehe mwanangu, sikujua haya yote yanaweza kutokea."

"Hapana mama, mimi wewe sikuweki kwenye hesabu hii, wewe uliingizwa kwenye mkumbo wa baba, pamoja na Doroth."

*******************************

Alioga, akala chakula. Akabadili nguo. Saa mbili na dakika tano, alitoka na kwenda kwenye sehemu ya kuegesha magari. Alichagua gari ambalo aliona litamfaa. Alijisachi na kuona bastola yake ipo sehemu sahihi aliohitaji. Aliingia kwenye gari, akawasha stati akaondoka.

Aliendesha kwa mwendo wa taratibu. Kiasi kwamba hata njiani alikuwa kero kwa baadhi ya madreva wengine.

Alitumia saa moja na kitu, kufika maeneo ya Namanga, wakati hakukuwa na foleni sana.

Aliisimamisha gari kwa mbali kidogo. Alikokuwa anakwenda alikufahamu vilivyo. Getini alimkuta mlinzi.

"Bito hujambo?" Alisalimia.

"Nani wewe?" Akaulizwa.

"Donald."

Mlinzi alionekana kushtuka.

"Vipi mbona umeshtuka?"

Mlinzi yule alikuwa anamfahamu Donald. Ingawa si mara nyingi alikwenda pale, lakini ni mtu ambaye kila anapofika pale kuwavunja mbavu, ambao mara nyingi huwa wawili wanaopeana zamu. Na akitoka ni lazima awaachie kitu kidogo.

"Samahani bosi amesema asiingie mtu." Mlinzi alisema, lakini maneno ambayo yalionekana kumtomridhisha Donald.

"Tangu lini mimi nimeanza kupangiwa masharti ya kuingia humu Bito?"

"Mama mwenyewe ndiyo kasema."

"Kwa hiyo kasema mimi nikija nisiruhusiwe au yoyote yule?"

"Yoyote yule."

Donald alianza kuhisi kuwa huenda ndani kukawa na kitu ambacho si cha kawaida.

Kila mmoja anafahamu kuwa yeye ni mpenzi wa Doroth, hivyo hakuna hata siku moja aliyozuiliwa.

"Sikiliza, chukua hii laki moja." Alichomoa noti kumi za shilingi elfu kumi.

"Niruhusu, halafu utawaambia kuwa sikupita getini, sawa?"

Bito alionekana kuafikiana na wazo hilo.

Haraka, Donald aliingia na kupenya kwa uangalifu mkubwa. Uzuri ni kwamba alikuwa akijua chumba kimoja baada ya kingine kwenye nyumba hiyo. Kabla ya kufika kwenye sehemu ya kulia chakula, alisikia maongezi. Kwa kawaida Doroth hukaa yeye, dada yake, na wafanyakazi wa ndani wawili, wa kike na wa kiume.

"Unasikia mpenzi, nia yangu ilikuwa ni kumaliza na kuchukua simu ili ushahidi ukosekane, lakini wale vijana niliowatumia kuna vitu walivikosea." Ilikuwa ni sauti nzito wa kiume.

"Chiko, wewe ndiyo umesababisha yote haya. Ni kweli Donald nilikuwa nampenda ni nilitaka anioe, tukamuua yule dada kwa kushirikiana na baba yake mzazi, lakini sasa mambo yamekuwa magumu. Donald anajua kila kitu, hii ni hatari hasa kwangu, Ndiyo maana nimeona niachane naye, lakini auawe ili wewe sasa uwe na mimi, lakini hili naona nalo kama linashindikana." Alisikia sauti ya Doroth ikilalamika.

INAENDELEA JUMAPILI



# Jitu Baya sasa mwendo 'Kazi Kazi' tu

RAPA anayewasha moto kila kukicha na kuwaogopesha wakongwe wa muziki huo, Jitu Baya, ameachia kibao chake kingine 'Kazi kazi' katika kutekeleza ahadi yake ya kutoa ngoma mfululizo.

Akizungumza na BT, Jitu Baya amesema wimbo huo amemshirikisha prodyuza maarufu FreshBoy, ni maalum kwa vijana wachapa kazi.

"Wimbo huu 'Kazi Kazi' ni maalum kwa vijana wanaochapa kazi, ni vizuri kila mtu akawajibika katika shughuli mbalimbali kwa ajili ya kujiingizia kipato kwani maisha si rahisi kama tunavyofikiria," amesema Jitu Baya.

Wiki mbili zilizopita mwanamuziki huyo alitambulisha ngoma yake nyingine inayoitwa 'Tunafika' akimshirikisha mwanamuziki chipukizi wa kike Aisha.

## Rhino The Don awamwagia mkwanja Nyamisifa

KUNDI la Nyamisifa limeibuka kinara katika shindano la Tingisha Challenge, linaloendeshwa na msanii anayeishi Marekani, Rhino The Don.

Rhino The Don, ameliambia gazeti hili kuwa kundi hilo limejipatia kiasi cha Sh. 500,000 kama zawadi baada ya kufanya vizuri kwa kucheza wimbo huo aliomshirikisha Nandy.

Akimshukuru Rhino The Don, C.E. O wa Nyamisifa Gang amesema : "Tunashukuru watu wote ambao walikubali kuandika ujumbe na kushiriki katika video zetu zote za shindano la Tingisha Challenge, hatimaye leo tumeshinda na kupata laki tano pia tunamshukuru director wetu kwa kufanikisha hili."



## ZISIKUPITE

### XAVI KUMRITHI KOEMAN

NYOTA wa zamani wa Barcelona, Xavi Hernandez huenda akachukua nafasi ya Kocha, Ronald Koeman aliye kwenye shinikizo la kuondolewa klabuni hapo. ***(Marca).***

### UNITED, RICE BASI

KLABU ya Manchester United inasaka mbadala wa kiungo wa England mwenye umri wa miaka 22, Declan Rice baada ya dau kubwa la pauni milioni 90 wanalolitaka West Ham kushindikana.(***ESPN***)

### RUDIGER KUTAJIRIKA

NYOTA Antonio Rudiger anaweza kujizolea mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki kama ataikacha Chelsea, huku klabu za Bayern Munich na Juventus zikiwa tayari kumpa mshahara huo mnono mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 28, kutoka ule wa pauni 130,000 kwa wiki anazolipwa sasa na Chelsea. (***Mirror***)

### MARTIAL ATAJWA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inamfuatilia mshambuliaji wa Manchester United Mfaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 25, kama mbadala wa mshambuliaji wake raia wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21. (***90min***)

### MBAPPE SOKONI RASMI

KLABU ya Manchester City inataka kuipiku Real Madrid katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22 msimu ujao. (***Transfer Window, via Mail***)

### MADRID YAIGOMEA ARSENAL

REAL Madrid ilikataa ofa ya Arsenal ya pauni milioni 34 ya kumsajili kiungo wake raia wa Hispania, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 25, msimu huu. (***Cadena Ser, via Mirror***)

### ATLETICO YAMFUATA SAKA

KLABU ya Atletico Madrid inataka mshambuliaji wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 22, Bukayo Saka. (***La Razon, via Star)***

### JAMES ATAKIWA

CHELSEA itataka wachezaji wanne kutoka Real Madrid kama mpango wa kumruhusu mlinzi wa kulia, Reece James mwenye umri wa miaka 21. (***Express***)

### KOUNDE MAMBO MAGUMU

KLABU ya Chelsea itaacha mpango wake wa kumwania mlinzi wa kifaransa kutoka Sevilla, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, na mlinzi wa kati wa PSG mbrazil, Marquinhos (27), ili kuelekeza nguvu zake za kumsajili mlinzi wa Juventus na Uholanzi mwenye umri wa miaka 22, Matthijs de Ligt. (***Star***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TAJIRI MAN CITY AMTAKA MBAPPE

●●● Afunguka yuko tayari kutoa kiasi chochote cha fedha ili kumnasa...

**MANCHESTER,** ENGLAND

KLABU ya Manchester City inaweza kuipiku Real Madrid katika mchakato wa kumsajili mshambuliaji, Kylian Mbappe kabla ya mkataba wake Paris Saint-Germain kumalizika mwisho wa msimu huu.

Mmiliki wa mabingwa hao wa England, Sheikh Mansour bin Zayed Al Nahyan ametoa mamlaka Mbappe awe miongoni mwa wachezaji wa klabu hiyo kwa gharama yoyote ile.

**Tajiri Mansour ametoa agizo uhamisho wa mfungaji bora wa PSG, Mbappe ukamilike mapema wakati wa dirisha dogo la usajili Januari 2022.**

Real Madrid inaonekana kukata tamaa kumsajili Mbappe baada ya maombi mawili kukataliwa kabla ya dirisha la usajili msimu wa joto kufungwa Agosti 31, mwaka huu.

Manchester City ilihusishwa kumsajili mmshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane msimu uliopita wa joto lakini iliripotiwa haikuwa tayari kulipa pauni milioni 150.

Mbappe mwenyewe hadi sasa bado hajakubali kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, jambo ambalo linamuweka kwenye nafasi nzuri ya kuondoka.

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI
HOME AWAY
ARSENAL
2.33 | 3.22 | 3.17
TOTTENHAM

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# AZAM YAINGIA 'KAZINI' KUIPELELEZA PYRAMIDS

**Na Saada Akida**

HUKU ikiwa na kibarua cha kupindua matokeo kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani dhidi ya Coastal Union katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema wanaendelea kuwafuatilia wapinzani wao katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Pyramids FC ya Misri.

Azam itacheza mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu kesho lakini inajiandaa kuwakaribisha Waarabu hao kati ya Oktoba 15 na 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Vivier alisema licha ya kukabiliwa na mechi ngumu dhidi ya Coastal Union, pia wanaendelea kujiimarisha kuelekea mchezo huo wa michuano ya kimataifa.

Vivier alisema mechi ya Pyramids itakuwa ngumu kwa ajili ya ubora wao na hali hiyo inawafanya wajiimarishe zaidi na mchezo dhidi ya Coastal Union utawaweka kwenye nafasi nzuri.

"Mechi hiyo itakuwa ngumu kwa ajili ya ubora wa wapinzani wetu, kikubwa tutakuwa tayari siku ya mechi dhidi ya pyramids ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, suala la kuwafuatilia ni lazima sana kwa kuwa mpira wa kisasa lazima ucheze na mtu unayemjuwa," alisema Vivier.

Azam FC imesonga mbele katika mashindano ya kimataifa baada ya kuwaondoa Horseed FC ya Somalia kwa ushindi wa jumla wa mabao 4-1.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (mwenye tai nyekundu), akiwa na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji na Bodi ya Wadhamini wa shirikisho hilo baada ya kumaliza kikao jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# *JKT Tanzania, Mwadui Kufungua Championship*

**Na Mwandishi Wetu**

MAAFANDE wa JKT Tanzania wataanza kampeni ya kurejea Ligi Kuu kwa kukutana na Mwadui FC kutoka Shinyanga katika mechi ya ufunguzi ya Ligi ya Championship itakayochezwa Oktoba 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Isamuyo, jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), jana inaonyesha ligi hiyo ambayo zamani ilijulikana kama Ligi Daraja la Kwanza itafunguliwa rasmi Oktoba 2, mwaka huu na itachezwa kwa mfumo wa nyumbani na ugenini.

Mechi nyingine zitakazochezwa siku ya ufunguzi zitakuwa ni kati ya African Lyon dhidi ya DTB wakati Pamba FC watawakaribisha Kengold kutoka Mbeya huku Ndanda FC wakiwavaa Kitayosce ya Tabora.

Oktoba 3, mwaka huu kutakuwa pia na michezo mingine ambayo Green Warriors itawaalika Transit Camp huku Gwambina FC itawafuata Ihefu kwenye Uwanja wa Highland Mbarali, Mbeya, African Sports itacheza dhidi ya Fountain Gate na Mashujaa FC itawakabili Pan African.

Ligi hiyo itakayotoa timu mbili zitakazopanda daraja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23 imepangwa kumalizika ifikapo Mei 21, mwakani.

LIVE IN PLAY

BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP

CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA

PAKUA SASA

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 26 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 2538 | Sparta Rotterdam vs Cambuur | 1.95 | 3.59 | 3.54 |
| 13:30 | 1495 | Juventus vs Sampdoria | 1.41 | 4.83 | 7.24 |
| 14:00 | 2601 | Bordeaux vs Rennes | 3.29 | 3.43 | 2.13 |
| 14:00 | 2978 | Dinamo Moscow vs Rubin Kazan | 1.86 | 3.45 | 4.04 |
| 14:00 | 4171 | St Mirren vs Aberdeen | 2.86 | 3.06 | 2.51 |
| 15:00 | 1845 | Mallorca vs Osasuna | 2.70 | 3.05 | 2.80 |
| 15:00 | 5448 | Midtjylland vs Randers | 1.60 | 4.03 | 4.92 |
| 15:15 | 1039 | FC Luzern vs FC Lugano | 2.26 | 3.46 | 2.91 |
| 15:30 | 4119 | AZ Alkmaar vs GO Ahead Eagles | 1.32 | 5.31 | 7.86 |
| 15:30 | 5623 | Heerenveen vs Twente | 2.31 | 3.35 | 2.91 |
| 16:00 | 2028 | Sassuolo vs Salernitana | 1.43 | 4.92 | 6.63 |
| 16:00 | 2045 | Udinese vs Fiorentina | 3.01 | 3.46 | 2.31 |
| 16:00 | 2260 | Brest vs Metz | 2.02 | 3.39 | 3.64 |
| 16:00 | 2525 | Hatayspor vs Fenerbahce | 3.05 | 3.40 | 2.21 |
| 16:00 | 3190 | Panathinaikos vs Volos | 1.53 | 3.89 | 6.11 |
| 16:00 | 4205 | Reims vs Nantes | 2.63 | 3.08 | 2.78 |
| 16:00 | 4490 | Southampton vs Wolverhampton | 2.63 | 3.18 | 2.78 |
| 16:00 | 4747 | Basaksehir vs Caykur Rizespor | 1.68 | 3.65 | 4.83 |
| 16:00 | 4778 | Troyes vs Angers | 2.68 | 3.13 | 2.68 |
| 16:00 | 5186 | Empoli vs Bologna | 2.62 | 3.63 | 2.52 |
| 16:00 | 5636 | Asteras Tripolis vs Olympiakos | 5.32 | 3.79 | 1.60 |
| 16:30 | 3568 | VfL Bochum vs Stuttgart | 2.94 | 3.49 | 2.28 |
| 17:00 | 5042 | KAA Gent vs Cercle Brugge | 1.39 | 4.83 | 6.71 |
| 17:00 | 5517 | Celtic vs Dundee Utd | 1.17 | 6.90 | 12.82 |
| 17:00 | 5537 | Hibernian vs St Johnstone | 1.85 | 3.40 | 4.14 |
| 17:15 | 5544 | Barcelona vs Levante | 1.50 | 4.62 | 5.85 |
| 17:30 | 1661 | Grasshoppers vs FC Sion | 1.88 | 3.70 | 3.65 |
| 17:30 | 2169 | FC Basel vs FC Zurich | 1.80 | 3.79 | 3.89 |
| 17:45 | 1278 | Heracles Almelo vs Waalwick | 1.81 | 3.65 | 4.05 |
| 18:00 | 2264 | Rapid Vienna vs Sturm Graz | 2.43 | 3.49 | 2.52 |
| 18:00 | 3829 | Clermont Foot vs Monaco | 3.58 | 3.53 | 1.99 |
| 18:30 | 1295 | SC Freiburg vs Augsburg | 1.87 | 3.49 | 4.09 |
| 18:30 | 4032 | Arsenal vs Tottenham | 2.33 | 3.22 | 3.17 |
| 19:00 | 2409 | Galatasaray vs Goeztepe | 1.50 | 4.25 | 5.73 |
| 19:00 | 4349 | Brondby vs Aalborg | 2.40 | 3.30 | 2.81 |
| 19:00 | 4631 | Lazio vs Roma | 2.62 | 3.43 | 2.62 |
| 19:00 | 5454 | FC Krasnodar vs Sochi | 2.07 | 3.45 | 3.30 |
| 19:30 | 2012 | Rayo Vallecano vs Cadiz CF | 1.61 | 3.90 | 5.61 |
| 19:30 | 3196 | Real Sociedad vs Elche | 1.43 | 4.41 | 7.62 |
| 19:30 | 3763 | Oostende vs Anderlecht | 3.89 | 3.89 | 1.78 |
| 20:00 | 3976 | Chicago Fire vs Nashville SC | 2.81 | 3.37 | 2.45 |
| 20:00 | 4084 | Slavia Prague vs Hradec Kralove | 1.17 | 6.83 | 16.06 |
| 20:00 | 5466 | Santa Clara vs Sporting Braga | 3.80 | 3.36 | 1.95 |
| 20:05 | 4553 | Hajduk Split vs Lokomotiva Zagreb | 1.51 | 4.14 | 5.20 |
| 20:30 | 5038 | PAOK vs AEK Athens | 2.23 | 3.21 | 3.16 |
| 21:45 | 2278 | Marseille vs Lens | 1.76 | 3.74 | 4.39 |
| 21:45 | 2694 | Napoli vs Cagliari | 1.27 | 6.03 | 10.05 |
| 22:00 | 3284 | Betis vs Getafe | 1.79 | 3.57 | 4.63 |
| 22:00 | 5528 | Racing Genk vs RFC Seraing | 1.31 | 5.52 | 7.68 |
| 22:30 | 4276 | Portimonense vs FC Vizela | 2.15 | 3.25 | 3.30 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# BARCELONA KUMREJESHA XAVI

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona inafikiria kumrejesha mchezaji wake wa zamani, Xavi Hernandez kama kocha mkuu wa klabu hiyo baada ya timu hiyo kuendelea kufanya vibaya msimu huu.

Xavi kwa sasa ni Kocha Mkuu wa klabu ya Al Sadd ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu Qatar, wakichukua ubingwa huo mara mbili mfululizo wakiwa na gwiji huyo.

Barcelona inayoongozwa na Ronald Koeman imekuwa na matokeo mabovu wakiwa wameshinda mechi mbili tu msimu huu kati ya tano walizocheza ikiwamo pia kupoteza nyumbani dhidi ya Bayern Munich katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Barcelona imepanga kumfukuza kazi kocha Koeman kutokana na matokeo mabovu wakati wanatarajiwa kuwa na kazi kubwa kumshawishi Xavi kurejea Hispania kutokana na familia yake kufurahia mazingira ya nchini Qatar.



# Liverpool yajitosa kumwania Haaland

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imejiunga kwenye msururu wa timu zinazowania huduma ya mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland kwa mujibu wa Sky Sport.

Mwanasoka huyo raia wa Norway ameendeleza pale alipoishia msimu uliopita akifunga mabao 11 katika mechi saba za mashindano yote.

Mshambuliaji huyo amekuwa nyota katika soka la ulaya tangu aliposhiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa klabu ya RB Salzburg mwaka 2019 kabla ya kujiunga na Dortmund.

Vigogo hao wa Ujerumani wamefanikiwa kumbakiza Haaland msimu huu licha ya Barcelona, Chelsea na Real Madrid kuonyesha dhamira ya kumsajili kwa vipindi tofauti.

Hata hivyo kwa sasa Chelsea inaonekana imesitisha nia kumwania mshambuliaji huyo baada ya kumsajili, Romelu Lukaku.

Gazeti la Mundo Deportivo la Hispania limesema hivi karibuni Haaland atakuwa kivutio zaidi kwa timu zenye nia kumsajili ambapo kipengele cha ada ya uhamisho kimeshuka hadi Euro milioni 90 sawa na Sh. bilioni 244.

# Michezo

Jumapili Septemba 26, 2021

Nipashe




Tajiri Man City amtaka Mbappe

UKURASA 21

# SIMBA SI KWA YANGA

## Wananchi wabeba Ngao ya Jamii kibabe baada ya miaka sita, Manara avua nguo uwanjani, Lwanga ala umeme...



**Na Waandishi Wetu**

BAO la dakika ya 11 la straika wa usajili mpya Fiston Mayele lilitosha kufuta rekodi mbaya ya miaka sita kwa Yanga kutobeba Ngao ya Jamii na kuendeleza ubabe dhidi ya watani wao wa jadi, Simba kwenye Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam jana.

Ikicheza kandanda la kuvutia lililochagizwa na pasi fupi zenye ubunifu na umahiri uliokosekana kwa miaka mingi inapokutana na Simba, Yanga iliibuka na ushindi huo wa tatu katika mechi nne walizokutana miezi tisa ya mwaka huu.

Watoto wa Jangwani walibeba Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar, wakiwazidi ujanja wa kupiga mikwaju ya penalti watani wao hao Januari 13, kisha kushinda goli 1-0 katika mechi ya watani ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara Julai 3 kabla ya kupoteza kwa bao 1-0 mjini Kigoma Julai 25.

Yote hayo yanatosha kuhalalisha tambo zinazotangazwa na mashabiki wake kwamba 'Simba si kwa Yanga bwana!'.

Nini kilitokea jana? Mayele, straika aliyesajiliwa msimu huu akitokea AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo (DRC), akicheza mechi yake ya kwanza kwenye kikosi cha Yanga, akiwa nje kidogo ya boksi, alipeleka simanzi kwa Wekundu wa Msimbazi, alipopiga shuti kali la kimo cha nyoka, akiunganisha kwa mguu wa kulia pasi murua iliyopenyezwa na kiungo Farid Mussa.

Kwenye mechi hiyo ambayo pengo la viungo washambuliaji Clatous Chama na Luis Miquissone lililonekana dhahiri ndani kikosi cha Simba, timu hiyo yenye maskani yake Kariakoo, haikucheza soka lake la kuvutia lililoshuhudiwa katika mechi nyingi zilizopita, zikiwamo za kimataifa.

Straika wake mwenye 'mwili jumba' Chris Mugalu alionekana kukosa umakini, akishindwa kutumia nafasi nne ambazo dhahiri zilikuwa na madhara kwa Yanga.

Mfungaji wa bao pekee la mechi ya Fainali ya Kombe la Shirikisho kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma, Thadeo Lwanga, alilazimika kutokuwa sehemu ya kikosi cha Mfaransa Didier Gomes kilichocheza dakika mbili za mwisho za mchezo huo baada ya kupata kadi ya pili ya njano kutoka kwa mwamuzi Ramadhani Kayoko, mkono wake wa kulia ulipoonekana ukitua usoni kwa Feisal Salum.

Kwa kushinda mechi ya jana, Yanga imeifikia rekodi ya Simba kutwaa Ngao ya Jamii mara ya sita. Mara ya mwisho Yanga kutwaa Ngao ya Jamii ilikuwa mwaka 2015 ilipoizidi Azam FC kwa matuta 8-7.

Mechi ya jana ilikuwa ya tano kwa watani hao kukutana kuwania Ngao ya Jamii, Wananchi wakishinda mara tatu na Simba mara mbili. Yanga iliifunga Simba mabao 2-1 mwaka 2001 na miaka tisa baadaye, yaani mwaka 2010, Wanajangwani walishinda kwa penalti 3-1.

Simba ilitwaa Ngao ya Jamii mwaka 2011 kwa kuifunga Yanga mabao 2-0 na 2017 kwa mikwaju ya penalti 5-4.

### MECHI ILIVYOANZA

Yanga waliuanza mchezo kwa kasi, wakipata kona sekunde chache za dakika ya kwanza, lakini haikuzaa matunda kama ilivyokuwa kwa kona zote walizopata jana.

Simba walijibu shambulizi katika dakika hiyo hiyo ya kwanza ya mchezo, Mugalu alipolisalimia lango la wapinzani wake kwa kuachia shuti la nje ya boksi baada ya kupewa pasi na Rally Bwalya, lakini mpira ukapaa juu la lango.

Khalid Aucho, kiungo mkabaji wa usajili mpya, alikuwa na nafasi ya kuipa Yanga bao dakika ya tano ya mchezo, lakini alichelewa kuutendea haki mpira wa krosi ya Jesus Moloko.

Nafasi kama hiyo aliipata Hassan Dilunga wa Simba dakika mbili baadaye, lakini shuti lake la mguu wa kushoto nje ya boksi lilimbabua Bakari Mwamnyeto na kusababisha kona.

Wachezaji wa Simba walishindwa kuukwamisha mpira wavuni, baada ya kona safi ya dakika ya nane iliyochongwa na Bwalya, beki wa kati Joash Onyango akiupiga kichwa mpira uliobabatiza mabeki wa Yanga kisha shuti lake likagonga mwamba na kuzua kizaazaa langoni hadi pale mabeki wa Yanga waliposimama imara na kuepusha balaa.

### MANARA AVUA

Baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, Haji Manara, alionekana akitembea kwa madaha na staili yake ya kukera, akifuatwa na waandishi wa habari waliokuwa wanampiga picha.

Katika kukoleza mbembwe zake, mtoto huyo wa straika wa zamani wa Yanga, Sunday Manara, alivua jezi aliyokuwa amevaa na kuirusha jukwaani, jambo lililotafsiriwa kama zawadi yake kwa mashabiki wa timu hiyo ya Jangwani.

### UWANJA WAPWAYA

Katika miaka ya karibuni, hiyo ni mechi ya kwanza iliyokosa 'amsha amsha' zilizozoeleka kwenye mechi zinazokutanisha vigogo hao wa soka nchini, mchezo huo ukipigwa siku chache baada ya sherehe ya Simba Day na Tamasha la Wananchi.

Hadi saa moja jioni, uwanja haukuwa na mashabiki wengi huku baadhi yao wakiwa nje ya uwanja, jambo ambalo halikuwa la kawaida kwa mechi zinazoikutanisha miamba hiyo ya soka nchini.

Makamu Mwenyeikiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema wamejipanga vizuri na kuifunga Simba kwao ni jambo la kawaida kwa sababu msimu uliopita waliondoka na pointi nne katika mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Kumfunga Simba kwetu ni kawaida, suala la kutufunga Kigoma ilikuwa ni bahati, ila kwa leo (jana) hachomoki, leo tunashinda ikiwa ni mwanzo wetu mzuri wa kuanza rasmi ligi," alitamba Mwakalebela dakika chache kabla ya kuanza kwa mechi hiyo.

Yanga walikuwa wa kwanza kufika uwanjani na baada ya kuingia ndani, walilazimika kupaki basi pembeni kwa dakika tano na kusubiri hadi Simba walipofika na kuingia ndani ya uwanja.

Simba waliingia uwanjani saa 9:27 alasiri na kuingia moja kwa moja sehemu maalum ya basi lao linapotakiwa kupaki na benchi la ufundi likiwa la kwanza kutoka ndani ya uwanja, huku beki wa kati Pascal Wawa, akianza kushuka upande wa wachezaji.

Dakika nane baadaye, yaani saa 9:35 alasiri, Feisal Salum 'Fei Toto' aliongoza wachezaji wa Yanga kushuka kwenye basi na waliingia uwanjani kwa kuukwepa mlango mkuu, wakipitia mlango wa chumba cha mikutano ya waandishi wa habari.

### VIINGILIO TATIZO

Baadhi ya mashabiki wa soka waliliambia Nipashe Jumapili kuwa sababu mojawapo ya uwanja kupwaya ni viingilio vya mechi hiyo kuwa vikubwa.

"Ni lazima TFF iangalie uhalisia, viingilio vya leo (jana) sio rafiki na mashabiki wa kawaida ndio huwapa pesa na kuongeza hamasa, watu wao wa VIP sio washangiliaji," alilalamika Shabani Mataka, shabiki wa soka.

Katika mechi ya utangulizi, timu ya mabalozi iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya viongozi wa dini. Mechi hiyo ililenga kuimarisha umoja na uhusiano.

***Imeandaliwa na Adam Fungamwango na Saada Akida**


9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042